# MATATIZO YA KUELEWANA KIMAONGEZI MIONGONI MWA WABALUHYIA WA MAGHARIBI MWA KENYA WANAOZUNGUMZA LAHAJA ZA KIISUKHA, KIKISA, KILOOGOLI NA KIBUKUSU.

NA

MUHATI PETER

TASNIFU HII IMETOLEWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA " MASTERS OF ARTS" KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

OKTOBA, 2002

University of NAIROBI Library
0479176 0

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe haijatolewa kwa mahitaji ya shahada Katika chuo kikuu kingine chochote.

Muhati Peter
(Mtahiniwa).

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu Mimi niliyeteuliwa na Chuo kuisimamia.

Prof M.H. Abdulaziz

23rd October 2002

**YALIYOMO** **UKURASA**

Ungamo

Yaliyomo

Tabaruku

Shukrani

Sura ya Kwanza

Utangulizi 2

Tatizo la utafiti 5

Madhumini ya Tasnifu 6

Nadharia tete 7

Sababu za kushughulikia tatizo 7

Upeo wa somo 8

Udarusu ya yaliyoandikwa kuhusu somo 9

Msingi wa nadharia 12

Mbinu za utafiti 14

Sura ya pili

Fonimu za Kiloogoli, Kiisukha,Kibukusu na Kikisa 16

Sura ya tatu

Tofauti za kileksika — 41

Sura ya Nne

Tofauti za kifono lojia katika lahaja — 75

Sura ya Tano

Tofauti za kimofolojia. — 86

Sura ya Sita

Tofauti za Kisimu jamii — 105

Hitimisho — 113

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe haijatolewa kwa mahitaji ya shahada Katika chuo kikuu kingine chochote.

________________________

Muhati Peter

(Mtahiniwa).

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu Mimi niliyeteuliwa na Chuo kuisimamia.

________________________

Prof M.H. Abdulaziz

## TABARUKU

Nawatabarukia tasnifu hii jamii za familia za Busula na Mango'ong'o kwa kuwa nami wakati Wote wa masomo yangu.

## SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani zangu kwa Prof. M.H Abdalaziz, Mwalimu wangu wa tasnifu hii. Aliweza kuniongoza na Kunielekeza kwa njia bora mpaka nikamaliza kuandika kazi yangu. Mola akubariki.

Pia sitawasahau wanafunzi wenzangu katika idara. Kwa upande wa somo la Kiswahili, tulikuwa na Amadi Adziaya, Magare Akeya, Mukoma Kamau na Ondeyo Ombegera.
Kwa upande wa somo la kiingereza kulikuwa na Gachigua Gakero, Maloba Wekesa Judy, Peris, Kingati, James Kigamwa. Hawa wote tulishirikiana nao kwa njia mbalimbali. Tulibadilisha mawazo mengi na kuvuta kamba hadi kufikia mwisho wa kazi yetu.

Vilevile ningependa kuwashukuru walimu wengine katika idara ya isumu na lugha za kiafrika kwa kazi nzuri waliofanya kunifunza.Hawa ni pamoja na Dr. Mbatiah, Dr Mberia, Dr. Mutiso, Bw Mgullu, Bw Arege, Bw Michira, Dr. Marete. Hongera nyote kwa kazi nzuri mliyoifanya.

Hali kadhalika sitawasahau bibi yangu Rhoda na mtoto Gladwell kwa uvumilivu Waliokuwa nao wakati wote nilipokuwa masomoni.
Mwisho ningependa kuwashukuru ndugu na marafiki wote walionipa usaidizi wa aina mbalimbali wakati wa masoma yangu. Ningependa haswa kumshukuru Timothy Ogada na ndugu yake Fred kwa kunisaidia kupiga chapa kazi yangu, Prisca Jerono na Grace Muthoni kwa kuipitia kazi yenyewe na kuikosoa na wengine wengi ambao sijawataja majina yao. Kwa nyinyi nyote nasema ASANTE SANA NA MUNGU AWABARIKI.

RAMANI YA KUONYESHA MAENEO WANAMOISHI WAISUKHA, WAKISA, WABUKUSU NA WALOGOOLI.




Kutoka kwa Angogo, (1983).

## 1.0 UTANGULIZI

Taifa la wabaluhya linapatikana Magharibi mwa nchi ya Kenya. Watu wanaozungumza Kibaluhya hupatikana hasa katika wilaya za Kakamega, Bungoma, Busia, Vihiga, Butere- Mumias na Lugari. Ingawa watu hawa huitwa Wabaluhya, hali halisi ni kuwa hakuna lugha ya Kibaluhya badala yake kuna lahaja mbalimbali ambazo hujumuishwa pamoja na watu wanaozungumza lahaja hizo kuitwa Wabaluhya. Watu hawa huzingatiwa kuwa wa kabila moja la Wabaluhya kwa vile wana historia moja, mila , desturi na tamaduni zinazofanana, wanaishi katika mazingara mamoja na vile vile wanazungumza lugha zinazokaribiana kiasi cha kuitwa lahaja za lugha ya Kibaluhya.

Wasomi wengi ambao wamewahi kuishughulikia lugha ya Kibaluhya wanakubaliana kuwa lugha hii ina lahaja kumi na saba[ Osogo(1966), Were(1967), William(1973), Itebete(1974), Angogo(1983), na Mojola(1999)] . Lahaja ambazo kwa jumla huunda kabila la Wabaluhya ni hizi zifuatazo:-

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kibukusu | Kimarachi | Kiisukha | Kitsotso | Kinyala(Busia) |
| Kitachoni | Kisamia | Kilogooli | Kikisa | |
| Kiwanga | Kikhayo | Kitiriki | Kikabras | |
| Kimarama | Kiidakho | Kinyala(kakamega) | Kinyore | |

Katika lahaja hizi kumi na saba, utafiti wetu utajishughulisha na lahaja nne peke yake ,nazo ni

Kiisukha, Kilogooli, Kikisa na Kibukusu.

Watu wanaoizungumza lahaja ya Kiisukha hupatikana katika wilaya ya Kakamega. Upande wa mashariki wanapakana na Wanandi, kaskazini na waluhya waongeao lahaja za Kikabras na Kitsotso. Upande wa Magharibi wanapakana na Waluhya wanaoongea Kiidakho ambao pia wanapakana nao upande wa Kusini. Lahaja ya Kiisukha inajumuisha koo mbalimbali zilizoungana pamoja(Were 1967). Waisukha ni miongoni mwa watu waliohamia eneo la Ubaluhya baina ya miaka 1598- 1733,baada ya kutoka maeneo walikoishi Wamaasai. Baada ya kuhamia maeneo ya Ubuluyia ,Waisukha walitupilia mbali lugha ya Kimaasai na kuanza kutumia Kisukha. Baadhi ya koo zinazounda jamii ya Waisukha ni Bamakhaya, Bimalia, Bamilonje, Bamahalia, Barimbuli, Bakusi, Bakhombwa, Bitsende, Baruli, Batsunga.

Kwa upande mwingine watu wanaoongea lahaja ya Kikisa walihamia eneo wanaloishi hivi sasa karibu wakati sawa na ule wa Waisukha(Osogo- 1966). Koo zinazojumuisha jamii ya Wakisa ni Abashisa, Abashibungo, Abashirotsa, Abasamia na Abakanga.

Nao Walogooli walihama kutoka eneo la mashariki mwa Uganda na kuingia sehemu ya Seme huko Nyanza ya Kati kabla ya kusonga hadi Maseno na mwishowe wakaingia katika maeneo wanamoishi sasa yaani Vihiga na Sabatia. Walogooli hupakana na

wabaluhya waongeao lahaja za Kitiriki, Kinyang'ori, Kinyore, na vile vile watu wanaoongea Kinandi na Kijaluo. Koo muhimu za Walogooli ni Abasali, Abakizungu, Abakirima na Abamaabi,(Osogo 1996).

Vilevile kuna lahaja ya Kibukusu. Kulingana na Simiyu(1985) na Makila(1978), chimbuko la watu wanaooongea lahaja ya Kibukusu ni Misri.Wasomi hawa wanaendelea kusema kuwa baada ya kutoka Misri, Wabukusu walienda mahali palipoitwa Embayi. Kutoka hapo walihamia sehemu ya Namarare karibu Mbale nchini Uganda kisha wakaenda Bubulo-Bukobelo na kwa muda mrefu waliishi katika vilima vya Bukusu katika mpaka wa Kenya na Uganda kabla ya kutawanyika katika maeneo wanakoishi sasa.

Idadi ya watu wanaozungumza kila lahaja tunazozitafiti kulingana na sensa ya 1999 ni kama ifuatayo:-

| LAHAJA | IDADI YA WATU |
|---|---|
| Kiisukha | 103, 948 |
| Kilogooli | 200, 858 |
| Kikisa | 111, 637 |
| Kibukusu | 876, 491 |

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Jami ya Waluyia kama jamii zingine za hapa nchini Kenya iliathiriwa na sera ya wakoloni wa Uingereza ya kutokubalia Waafrika kuhamahama kutoka eneo moja hadi lingine kwa urahisi. Hata hivyo ,baada ya Wakenya kujinyakulia uhuru ,jambo hili lilifutiliwa mbali na watu wanaoongea lahaja mbalimbali za Kibaluyia sawa na watu wa jamii zingine nchini wakakubaliwa kuhamia maeneo waliyoyataka bila pingamizi. Jambo hili limezidishwa katika siku za hivi karibuni katika jamii ya Waluyia sambamba na jamii zingine za Kenya kwa kuhamiswa kila mara kwa maafisa wa serikali ili kuleta utangamano katika nchi yetu iliyojaa watu wanaozungumza lugha na anuwai za lugha tofauti.,

Hatua hizi zimeimarishwa na sera sambamba ya serikali ya kuwakubalia wanafunzi wa shule shule za msingi na upili wanaotoka katika maeneo tofauti ambapo lugha na anuwai tofauti za lugha huongewa kuweza kusomea pamoja. Vilevile tusisahau kutaja hapa kuwa walimu hupelekwa kufunza katika maeneo ambapo lugha zinazotumiwa na wenyeji sio lugha zao za kwanza.Kuongezea kwa hayo mabadiliko ya kisiasa yamewafanya watu wanaoongea lahaja tofauti za kiluyia kuweza kuzitumia lahaja hizo tofauti wakiwa katika kikao au vikao mbalimbali ili kujitambua kama watu wa jamii moja yaani jamii ya Waluyia walio na msimamo mmoja wa kisiasa. Hatua hizi zote zinamaanisha kuwa kunatakiwa kuwe na maarifa ya
au uwezo fulani wa ufahamu wa lahaja ya wenyeji kwa mtu asiye mzungumzaji asilia wa lahaja hiyo.

Haya yote yanatuelekeza katika kujibu swali moja muhimu

Je ni matatizo yapi ya kimawsiliano ambayo mtu asiyeongea lahaja asilia ya wenyeji anapata katika mazingira ambapo hawezi kutumia lahaja yake ya kwanza au Kiswahili wala Kiingereza?

Wasomi wa hapo awali ambao wamewahi kuitafiti lugha ya Kiluyia [ Tazama kazi za Lidonde(1976), Magwaga(1989), Mebo(1989), Itebete(1974), Angogo(1983) ],hawajashugulikia swala hili na kwa hivyo kutufanya kulichunguza. Hata hivyo kwa vile jamii ya Waluyia ina wawzungumzaji wa lahaja nyingi( kumi na saba ) hatutaweza kuzishughulikia lahaja hizo zote bali tutazishughulikia nne pekee yake yaani lahaja za Kibukusu, Kilogooli , Kikisa na Kiisukha.

## 1.2 MADHUMUNI YA TASNIFU.

Lengo kuu la tasnifu hii ni kuthibitisha ya kwamba matatizo ya kimawasiliano hutokea wakati watu wanaozungumza lahaja za Kiisukha, Kikisa, Kilogooli na Kibukusu wanapoongea.

Utafiti huu unadhamiria kutimiza lengo hili kupitia njia zifuatazo:-

1) Kuonyesha tofauti za kilekisika miongoni mwa maneno ya lahaja hizi nne yaani Kiisukha, Kikisa, Kilogooli na Kibukusu.

2) Kuonyesha tofauti za kimatamshi ya maneno katika lahaja hizi.

3) Kubainisha tofauti za kimofolojia za maneno katika lahaja hizi

4) Kueleza baadhi ya mambo ya kiisimu-jamii yanayochangia katika kutatiza mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja hizi.

## 1.3 NADHARIA TETE.

Tasnifu hii inazo nadharia tete zifuatazo:-

a) Kwamba miundo tofauti ya kimofolojia na kifonolojia ya maneno ndiyo inayoleta matatizo mengi ya kimawasiliano miongoni mwa watu wanaozungumza lahaja za Kiisukha, Kikisa, Kilogooli na Kibukusu.

b) Kwamba tofauti za kileksika pia zimechangia katika kutatiza mawasiliano ya kimaongezi miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja hizi za Kiisukha, Kikisa, Kilogooli, na Kibukusu.

c) Kwamba tofauti za miundo ya maneno miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja hizi zaweza kusababisha ugumu kwa msemaji wa lahaja fulani anayejaribu kuimudu lahaja nyingine.

d ) Kwamba taasubi zinazoshikiliwa na watu wanaoongea lahaja fulani zimechangia katika kurahisisha au kutatiza kabisa mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja hizo nne.

## 1.4 SABABU ZA KUSHUGHULIKIA TATIZO.

a)Utafiti huu ni muhimu kama mchango wa usomi.Utafiti wa kiulinganishi ni sehemu muhimu ya isimu kwa ujumla wake kama somo na huongezea uelewaji wetu wa uendelezaji wa mahusiano miongoni mwa lugha za ulimwengu.Kwa hivyo utafiti huu

utaongezea habari iliyoko kuhusu lugha ya Kiluhya kwa ujumla na hasa lahaja tutakazo zizingatia.

b)Mtafiti wa kazi hii ni mzungumzaji asilia wa mojawapo ya lahaja zitakazofanyiwa utafiti(Kiisukha).Kuichagua lahaja hii kama mojawapo ya zile zitakazofanyiwa utafiti kunaoana na pendekezo la mwanaisimu Milroy(1987) anayesema kwamba umilisi wa lugha ya sehemu ya utafiti ni muhimu katika utafiti wa kiisimu. Isitoshe mtafiti ameishi miongoni mwa watu wanaoongea Kiluhya kwa zaidi ya miaka ishirini. Kwa hivyo ana tajriba ya kutosha katika lahaja ya Kiisukha na ameshuhudia matatizo mbalimbali yakitokea wakati watu wa lahaja tofauti za Kiluhya wanapowasiliana, jambo lililomsukuma kufanya utafiti wa aina hii.

c)Hakuna utafiti wa aina hii uliofanywa hapo awali. Hakuna wanaisimu au wasomi wengine

wa hapo awali waliolinganisha lahaja hizi nne wakiwa na nia ya kubainisha matatizo ya kimawasiliano yanayotokea wakati watu wanaozungumza lahaja za Kiisukha, Kikisa, Kilogooli na Kibukusu wanapoongea.

d)Watu wanaoongea lahaja za Kilogooli na Kibukusu hudai kuwa hawaelewani kwa kiwango kikubwa sana(Angogo 1983). Lahaja ya Kikisa imeorodheshwa kama mojawapo ya lahaja za kati. Sifa hii inaipa lahaja hii uwakilishaji mpana wa lugha ya kibaluhya (Itebete katika Whiteley 1974). Kiisukha ndio lahaja anayoizungumzia mtafiti.Vilevile mtafiti anazifahamu lahaja za Kilogooli na Kikisa kwa asilimia themanini hivi na pia kuifahamu lahaja ya Kibukusu kwa asilimia sabini na tano hivi. Mambo haya

yanafanya lahaja hizi kuweza kulinganishwa na maamuzi yafaayo kuafikiwa kutokana na ulinganishi huo.

## 1.5UPEO WA SOMO HILI.

Utafiti huu unalenga lahaja za kibaluhya nne. Lahaja hizi ni Kiisukha, Kilogooli, Kikisa na Kibukusu.

Maswala yanayolengwa ni yale ya kiisimu. Tutajikita katika maswala ya kimuundo ya lahaja hizi, kwa mfano kuwepo au kutokuwepo kwa baadhi ya sauti katika lahaja moja ikilinganishwa na nyingine.

Tofauti za njeo na za minyambuliko pia zitazingatiwa.

Vilevile utafiti huu ni wa kiuainishi , hatutazingatia maswala ya kihistoria ya lahaja hizi. Licha ya haya, utafiti wetu utazingatia swala la isimu-jamii kuhusu misimamo tofauti inayoshikiliwa na waongeaji wa lahaja moja dhidi ya wenzao wanaozungumza lahaja tofauti.

## 1.6 UDURUSU WA YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI.

Kuna kazi aina mbalimbali za kiisimu, kihistoria na kianthropolojia ambazo ni muhimu kwa utafiti huu. Kazi za kihistoria na kianthropolojia zitakuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile zitatusaidia kupata habari kuhusu chimbuko na historia za wazungumzaji wa lahaja hizi nne yaani Kiisukha, Kikisa, Kilogooli na Kibukusu. Nazo kazi za kiisimu zitachangia utafiti huu kwani maswala tutakayozingatia ni ya kiisimu.

Kazi za kihistoria za Osogo(1966) na Were(1967) zitakuwa muhimu kwa utafiti huu kwa vile zitatusaidia kupata historia fupi fupi za kila lahaja iliyozingatiwa katika utafiti huu. Ingawa walitegemea sana masimulizi waliyoambiwa na wazee waliozungumza lahaja mbalimbali, yale waliyoyakusanya yatatuangazia kuhusu kabila la Wabaluhya kwa ujumla. kwa upande mwingine kazi za kianthropolojia za Wagner (1949 na 1954) zitatusaidia kuielewa jamii ya Waluyia vyema zaidi

Miongoni mwa kazi za hapo awali ni ile ya Johnson (1919 ) Acomparative study of the Bantu and semi Bantu languages. Mwandishi anaorodhesha hoja kumi na moja ambazo anaeleza kuwa zina upekee wake kwa lugha za kibantu. Kulingana naye lugha za kibantu zina uhusiano wa karibu unaoonyesha mfanano wa kifonolojia, kileksika, kisintaksia na

kimofolojia.Jambo hili ,kulingana na Guthrie (1967 ) linafanya lugha hizo kuweza kufanyiwa utafiti wa kiulinganishi.Hoja alizotaja Johnson ni nzuri na zaweza kutumika kuunda nadharia tete muhimu ambazo zaweza kuelekeza katika utafiti mwingine. Hata hivyo kwa vile kazi ya Johnson ilihusisha ulinganishi baina ya makundi ya kibantu kamili na yaliyo nusu Bantu, kazi hiyo ni ya kijumla na haitupi habari za undani kuhusiana na kila lugha binafsi.

Kumekuwa pia na utafiti uliozingatia lahaja mbalimbali binafsi. Utafiti wa aina hii ni muhimu kwa vile njia zilizotumiwa zinaweza pia kutumika katika kuzichunguza lugha au lahaja zingine. Kwa mfano kazi ya Brown (1972 ) Phonological rules and dialect variation; A study of the phonology of Lumasaaba ambapo amezilinganisha Kibukusu

na Kigishu ni jambo linalohusiana na utafiti wetu. Uchunguzi wake uliweza kubainisha kuwa wazungumzaji wa Kibukusu na Kigishu wanaelewana kwa kiwango kikubwa sana. Mbinu aliyoitumia ya takwimu leksika itatumika katika utafiti wetu wakati wa kufanya uchanganuzi wa kileksika.

Tasnifu ya Dalgish (1976 ) A study of the morphophonemics of Luhya dialectss , inachunguza lahaja ya Kitsotso. Kazi yake inaweza kutumika kama kirejeleo wakati wa kuzifanyia utafiti mofolojia za lahaja zingine za Kiluyia na pia lugha zingine zilizo na uhusiano wa karibu na kiluyia. Kwa hivyo mbinu alizotumia na uchanganuzi alioufanya unatupa mwanga kwa lahaja tunazozichunguza katika utafiti wetu.

Kazi zingine muhimu ni zile za Makila(1978) na Simiyu(1985).Kazi hizi zimeangazia historia ya Wabukusu na zitatusaidia kuelezea historia hiyo kwa ufupi. Hali kadhalika kazi ya Itebete(1974) ni ya umuhimu kwetu. Kazi hii imezingatia sababu zilizoelekeza makundi mbalimbali kama vile wamishonari kufikiria kuhusu swala la uwezekano wa kuwepo kwa othografia ya aina moja ya Kibaluhya. Pia imezingatia utafiti ambao ulipaswa kufanywa kabla ya usanifishaji wa lugha ya Kibaluhya. Vilevile Itebete [1974] amezungumzia pingamizi kutoka sehemu mbalimbali dhidi ya usanifishaji huo na kutaja baadhi ya tofauti za kimsamiati miongoni mwa lahaja tofauti za Kibaluhya. Kwa ujumla twaweza kusema kuwa kazi hii ni muhimu kwetu kwani yaangazia tatizo la mawasiliano katika kiwango cha maandishi na kwa hivyo kutufanya kufikiria kuhusu tatizo la mawasiliano katika kiwango cha masimulizi.

Kazi ya Angogo(1983) ni muhimu sana kwa utafiti wetu. Mwandishi huyu amezungumzia maswala ya kijumla ya kifonolojia, kimofolojia, kileksika na kisintaksia ya lahaja tofauti za Kibaluhya huku akionyesha jinsi zinazofanana au kutofautiana. Pia anataja tofauti za kiothografia zilizotokana na kuandikwa kwa Bibilia. Anataja juhudi za usanifishaji wa lahaja mbalimbali za Kibaluhya zilizofanywa hapo awali. Kuongezea kwa hayo anatupa data kuonyesha viwango vya uelewanaji miongoni mwa lahaja hizo, yaani Agongo anaonyesha ikiwa wazungumzaji wa lahaja tofauti anaelewana kwa karibu au kwa umbali.

Utafiti wetu waanzia hapo kwa kutaka kujua matatizo ya kimawasiliano yanayoletwa na viwango hivi tofauti vya uelewanaji. Hata hivyo, kwa vile kazi ya Agongo(1983) imezingatia lahaja zote za kibaluhya kwa ujumla, kazi yake haikuingilia maswala anayoyataja kwa kina na maki . Kazi zingine zilizoshughulikia lahaja mbalimbali za Kibaluhya ni tasnifu kama zile za Mebo (1989), Magwaga(1989) na Lidonde(1976). Ingawa kazi hizi zimeshughulikia maswala ya kimofolojia, fonolojia na sintaksia ya lahaja tofauti-tofauti za kibaluhya, kazi hizi zimefanikiwa kutoa mwanga kuhusu miundo tofauti ya lahaja zilizoshughulikiwa kwani katika kazi hii twataraji kushughulikia miundo ya maneno katika lahaja za Kiisukha, Kilogooli, Kikisa na Kibukusu.

## 1.7 MSINGI WA NADHARIA.

Kazi yetu imejikita katika misingi ya isimu linganishi. Isimu linganishi hujumuisha lugha (au anuwai za lugha ) mbili au zaidi ili kuweza kufikia maamuzi ya kiisimu kuhusiana na lugha au anuwai hizo za lugha.(Robins 1980 ).

Isimu linganishi imegawanywa katika matawi mawili makuu. Tawi la kwanza ni isimu linganiishi kihistoria . Hili ni tawi ambalo hujishughulisha na kutoa maamuzi kuhusu maendeleo ya kihistoria ya lugha (au anuwai za lugha ). mbili au zaidi, ikiwa na lengo la kuonyesha lugha zazi ya lugha (au anuwai za lugha husika ). Ulinganishi wa aina hii wa kidayakronia ulikuwa maarufu sana katika karne ya kumi na tisa ambapo wasomi walichunguza mahusiano baina ya familia za lugha kama vile Sansikiriti , Kigiriki ,na Kilatini ili kuweza kubaini lugha zazi zao.

Tawi la pili la isimu linganishi ni lile la isimu linganishi kiuainishi (kitaipolojia )Tawi hili hujishughulisha na kuonyesha tofauti au kulingana kwa miundo, maumbo na sifa mbalimbali baina au miongoni mwa lugha (au anuwai za lugha), lengo kuu likiwa ni kutuonyesha mahusiano au tofauti za kiisimu bila kuzingatia historia ya lugha hizo (au anuwai za lugha). Mmojawapo wa waasisi wa isimu linganishi kiuainishi ni mwanaisimu Mjerumani aliyeishi katika karne ya kumi na nane , Wilheim Von Humboldt. Yeye alizigawanya lugha katika makundi matatu, yaani lugha ambishibainishi, lugha tenganishi na lugha ambishi mchanganyo. Uainishaji wa aina hii uliweza kutumiwa na wanaisimu wa karne ya ishirini, miongoni mwao akiwa Sapir aliyeitumia mbinu hiyo katika kitabu chake kilichochapishwa mwaka wa 1921, Language . Katika miaka ya hivi karibuni mwanaisimu Greenberg ameziainisha lugha mbalimbali kwa kuzingatia misingi hii ya isimu linganishi. Utafiti wetu utazingatia ulinganishi huu wa kiuainishi.

Tutazingatia pia nadharia ya kisaikolojia ya jamii kuhusiana na kujifunza lugha ya pili. Nadharia hii iliasisiwa na Lambert.W.E (1963). Yeye alielezea ifuatavyo:-

*"Nadharia hii kwa muhtasari hushikilia kwamba mtu anayetaka kuimudu lugha au anuwai ya lugha ya pili.,hujaribu kuiga mambo fulani ya kitabia yanayobainisha watu walio katika kikundi hicho cha kiisimu. Mielekeo yake kuhusu kabila lake na misimamo(hisia) yake kuhusu watu wanaozungumza lugha anayojaribu kuimudu ndizo zitakazoamua ufanisi wake katika kujifunza lugha hiyo ya pili. Kwa hivyo tunaona kuwa motisha ya kutaka kujifunza na kuimudu lugha ya pili hutokana na misimamo(hisia) aliyonayo kuhusiana na lugha hiyo na jinsi anavyoichukulia lugha hiyo kwa ujumla".*

Nadharia hizi mbili zitatufaa katika utafiti wetu unaoshughukia miundo na swala la taasubi kuhusu lahaja za Kibaluhya.

**1.8 MBINU ZA UTAFITI.**

Katika utafiti huu watu wa jinsia zote watazingatiwa. Hata hivo watagawanywa katika makundi matatu makuu.

Kundi la kwanza litawahusisha vijana wa kiume na wa kike wa umri kati ya miaka 18-25. Idadi ya wahusishwa itakuwa watu 30 ambapo vijana wa kiume 15 na wa kike 15 kutoka kila lahaja watahusishwa.

Kundi la pili litakuwa la wanaume na wanawake walio na umri wa kati ya 30- 45 kutoka kila lahaja. Idadi ya wahusishwa hawa itakuwa sawa na ile ya kundi la kwanza.

Nalo kundi la tatu litakuwa ni la wanaume na wanawake walio na umri wa miaka kati ya 50- 55kutoka kila lahaja na idadi yao itakuwa sawa na ile ya kundi la kwanza na la pili.

Ugawanyaji huu utatuwezesha kuwa na sampuli ya kutosha ya kuwakilisha watu wa jinsia na umri mbalimbali na wa lahaja zote. Kwa hivyo ugawanyaji huu utawezesha kufikia uamuzi unaofaa.

Mbinu zifuatazo zitatumika katika utafiti huu:-

a) Kunasa mazungumzo ya wazungumzaji kutoka kila kikundi cha lahaja hizo nne, yaani Kibukusu, Kikisa, Kiisukha na Kilogooli.Baada ya kunasa sauti tutaweza kuchanganua mazungumzo hayo.

b) Wazungumzaji kutoka kila kikundi na kutoka katika kila lahaja watachaguliwa ili waweze kusikiliza na kutafsiri aina moja ya makala kutoka lugha ya kiswahili au kiingereza hadi lahaja zao tofauti. Tafsiri zao zitaweza kuchanganuliwa kwa misingi ya kisiimu ili kubainisha tofauti za kimofolojia na kifonolojia.

c) Orodha ya msamiati wa kimsingi katika lahaja zote itanakiliwa kutoka kwa wazungumzaji wa lahaja hizo kutoka kila kikundi.Baadaye mbinu ya takwimu leksika itatumika katika uchanganuzi wa kileksika ili kuweza kubainisha tofauti za kileksika miongoni mwa lahaja hizo.

d) Utafiti utafanywa maktabani ambapo vitabu mbalimbali vya isimu vitatumiwa ili kuongezea kwa yale yatakayokusanywa kutoka kwa wazungumzaji wa lahaja hizi.

e) Utafiti wa kiisimu- jamii utafanywa kwa kutumia hojaji

f) Katika uchanganuzi, ulinganishi utafanywa kwa kuzingatia lahaja zote nne ili matatizo ya mawasiliano ya kimaongezi miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja hizo yaweza kujitokeza waziwazi.

# SURA YA PILI

## FONIMU ZA KILOOGOLI, KIISUKHA, KIBUKUSU AND KIKISA

### 2.1 Utangulizi

Fonimu ni kama ishara ambazo huambatana kwa mpangalio maalum ili kuumba maneno yenye maana mbalimbali. Kwa mujibu wa Hjelmsler (1970), mahusiano ya ishara hizi kwa kutii kanuni maalum ndiyo msingi wa mfumo au muundo wa lugha yoyote ile. Hizi ishara zinaweza kuwakilishwa kifonetiki. Kila moja ikapewa unukuzi makinifu unaobainisha kama sauti inatofautiana na sauti nyingine za lugha hiyo. Kwa mujibu wa Gleason (1955) haiwezekani kuchunguza muundo wa kiisimu wa lugha yoyote ile bila kwanza kuzijua fonimu zake. Kutokana na maelezo hayo, fonimu konsonanti na fonimu irabu zifuatazo zimeorodheshwa kwa kila lahaja.

### 2.2 KILOGOOLI

Kilogooli kina jumla ya fonimu 31, 24 zikiwa ni fonimu konsonanti na 7 zikiwa ni fonimu irabu.

| | Midomo | Midomo meno | Ufizi | Kaakaa | Kaakaa laini | Glota |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipasuo | b | | d | | g k | |
| | | | t | | ŋ | |
| Nazali | m | | n | r | | |
| Kitambaza | | | | l | | |
| **Kimadende** | | | r | | | |
| **Kipigo** | | | z | | | |
| | | | s | | | |
| **kikwamizwa** | b | f | | j | | h |
| **Kizuiwakwamizwa** | | | | d | | |
| **kifulzwahuru** | | | | | w | |
| **Sauti mlolongo** | mb | n d | nz | ɲdʒ | | |
| | | [illegible] | | | | |

Sauti /r/ huchukuliwa kuwa kibadala cha sauti / / kwa vile sauti / / hutumika sana kuliko sauti /r/ na pale ambapo sauti /r/ hutumika haitamkwi waziwazi kama /r/, isipokuwa kwa

maneno machache pekee. Kwa hivyo fonimu konsonanti za Kilogooli ni kama zifuatazao.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | /m/ | Katika | Maduma (mahindi) |
| | | | Mavele (Maziwa) |
| 2. | /d/ | Katika | deka (pika) |
| | | | duya (gonga) |
| 3. | /j/ | katika | yeya (pangunza) |
| | | | yeyo (hapo/kule) |
| 4. | /h/ | katika | hanu (hapa) |
| | | | henza (angalia/tazama) |
| 5. | /ŋ/ | katika | ng'avula (panua) |
| | | | ng'ano (kumbe) |
| 6. | /ɲ/ | katika | nyenya (nataka) |
| | | | linyonyi (ndege) |
| 7. | /k/ | katika | kina (cheza) |
| | | | kale (kitambo) |
| 8. | /g/ | katika | gona(lala) |
| | | | gaya (kataza) |
| 9. | /t/ | katika | tula (toka) |
| | | | tuma (ruka) |
| 10. | /z/ | katika | Zimoni (macho) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Zisoni (aibu) |
| 11. | /n/ | katika | nina (panda) |
| | | | nuuna (nyonya) |
| 12. | /ɭ/ | katika | mulala (mmoja) |
| | | | halala (pamoja) |
| 13. | /r/ | katika | reta (lete) |
| | | | rota (ota) |
| 14. | /l/ | katika | buli (wote) |
| | | | babili (wawili) |
| 15. | /f/ | katika | kufwana (kufanana) |
| | | | kifwoyo (sungura) |
| 16. | /s/ | katika | sambaga (choma) |
| | | | isambakulu (kiwashaji) |
| 17. | /w/ | katika | kinanwa (kidevu) |
| | | | munwa (mdomo) |
| 18. | /ŋg/ | katika | inguruvi (nguruwe) |
| | | | ingurumani (maini) |
| 19. | /nz/ | katika | inzira (njia) |
| | | | inzara (njaa) |
| 20 | /dʒ/ | katika | ijumbi (chumzi) |
| | | | jaaga (anzisha) |
| 21 | /mb/ | katika | indumba (ngoma) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | mirembe (salamu) |
| 22. | /ɲʒ/ | katika | njeriza (nisabamu/nijaribu) |
| | | | njuyi (nimerudi) |
| 23 | /nd/ | katika | inda (tumbo) |
| | | | indu (nini) |

## FONIMU VOKALI



| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | /I/ | katika | ikidaho (kidimbwi) |
| | | | ikisungigu (bakalo) |
| 2. | /I/ | katika | umwayi (mchungaji) |
| | | | Umwimali (msichana katika harusi) |
| 3. | /ɛ/ | katika | degela (tetemeka) |
| | | | dengeya (hafifu) |
| 4) | /a/ | katika | samba (choma) |
| | | | sandula (chapa kofi) |
| 5) | /u/ | katika | umukuyu (aina ya mti) |

uyu (huyu)

6) /ʊ/ katika tuuma (ruka)

duumula (haribu)

7) /ɔ/ katika yaho (hapo)

yecho (hicho)

Kuna vokali ndefu na fupi na mlingano huo ni wa kifonemiki. Kwa mfano

1) heenza - /he:nza/ - angalia

henza - /henza/ - onyo

2) tuuma - /tu:ma / - ruka

tuma /tuma/ - tuma

3) taaga - /ta:ga - panda

taga - /taga/ - tega

Mlolongo wa konsonanti katika Kilogooli ni ule unaohusisha nazali. Muungano huo unaelekezwa na sifa za kifonetiki za konsonanti husika. Konsonanti mbili zinazofuatana

lazima ziwe na sifa moja ya kifonetiki, kwa mfano sifa ya mahali pa kutamkia sauti, mfano

m + b = mb inakubalika

m + d = md haikubaliki

Sauti m na b zinaweza kuunda mlolongo wa konsonanti kwa vile zote ni sauti zinazotamkwa midomoni

## 2.3 KIISUKHA

Lahaja ya Kiisukha ina jumla ya fonimu 31, fonimu konsonanti 24 na fonimu irabu 7, kama inavyoonyeshwa katika jedwali ifuatayo.

**Fonimu - Konsonanti za Kiisukha**

| | midomo | Midomo meno | Ufizi | kaakaa | Kaakaa ufizi | Kaakaa laini | Glota |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipasuo | p | | t | | | k | |
| nazali | m | | n | ɲ | | ŋ | |

| | Midomo | Midomo meno | Ufizi | Kaakaa | Kaakaa ufizi | Kaakaa laini | Glota |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kitambaza | | | | l | | | |
| | | | r | | | | |
| kikwamizwa | B | f | s | j | | | h. x |
| kizuiwakwamizwa | | | ts | t | | | |
| Kifululizwa huru | | | | | | w | |
| mlolongo | mb | | nd<br>nz | ɲ dʒ | | ŋg | |

1) /k/ katika kula (nunua)
kora (potea)

2) /n/ katika nuna (nyonya)
vuna (peleleza)

3) /ŋ/ katika ing'ombe (ng'ombe)
ling'ondo (peni moja)

4) /ɲ/ katika inyungu (nyungu)
inyanya (nyanya)

5) /m/ katika maroi (masikio)
matoi (matope)

6) /b/ katika Bwongo (akili)
bindu (vitu)

7) /r/ katika rula (toka)

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | reka (teka) |
| 8) | /f/ | katika | fwana (fanana) |
| | | | fwala (vaa) |
| 9) | /ɺ/ | katika | lola (ona) |
| | | | lula (kuwa mkali) |
| 10) | /s/ | katika | sunda (songeza) |
| | | | saala (omba) |
| 11) | /h/ | katika | hasi (chini) |
| | | | hosi (kote) |
| 12) | /ʃ/ | katika | shirula (cha kutoka) |
| | | | shieyo (kifagio) |
| 13) | /j/ | katika | yeka (kuna) |
| | | | yoko (kama) |
| 14) | /x/ | katika | khutsa (kufa) |
| | | | khaatsa (tafuna) |
| 15) | /p/ | katika | khupa (piga) |
| | | | pulukha (paa angani) |
| 16) | /t/ | katika | tola (okota) |
| | | | taala (zunguka) |
| 17) | /ts/ | katika | tsisendi (pesa) |
| | | | tsisala (vijiti) |
| 18) | /ʧ/ | katika | chelitsa (jaribu) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | chenda (tembea) |
| 19) | /w/ | katika | weeka (ulijifunza) |
| | | | wosi (wowote) |
| 20) | /mb/ | katika | samba (choma) |
| | | | hamba (kuja) |
| 21 | /nz/ | katika | yanza (furahi) |
| | | | henza (angalia) |
| 22) | /nd/ | katika | mandu (takataka) |
| | | | inda (tumbo) |
| 23) | /ɲdʒ/ | katika | injila (njia) |
| | | | injelosi (malaika) |
| 24) | /ŋg/ | katika | panga (panga) |
| | | | runga (lipa) |

## Vokali

Vokali za Kiisukha ni sawa na zile za Kilogooli ( Tazama jedwali ya vokoli za Kilogooli).

Vokali zifuatazo zimeorodheshwa

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1) | | katika | mwiri (muuaji) |
| | | | mwibi (mwizi) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2) | /ɪ/ | katika | linda (ngoja) |
| | | | lima (homa) |
| 3) | /ɛ/ | katika | leka (kasirika) |
| | | | reka (tega) |
| 4) | /a/ | katika | raaka (panda) |
| | | | hamba (kuja) |
| 5) | /ɔ/ | katika | ronya (anguka) |
| | | | moola (tamba) |
| 6) | /ʊ/ | katika | muliru (msitu) |
| | | | hula (piga) |
| 7) | /u/ | katika | hanu (hapa) |
| | | | mundu (mtu) |

Irabu hutokea mwanzoni mwa neno ambayo pia ni kiambishi awali lakini huwa ni nadra sana katika lahaja hii yaKiisukha kinyume na lahaja ya logooli, kwa mfano

Kilogooli - Umuundu (mtu)

Kiisukha - Mundu (mtu)

Hali kadhalika kuna irabu fupi na zile ndefu kwa mfano>

1) ruma - /ruma/ - tuma

ruuma - /ru: ma/ - ruka

2) yeka - /jɛka/ - kuna

yeeka - /jɛ:ka/ - alisoma

3) Yitsi - /jitsi/ - hizi

Yiitsi - /ji:tsi/ - amekuja

4) Nyola - chuna mboga

Nyoola - pata

5) Mala - matumbo

Maala - songa

Urefu au ufupi wa vokali linaweza kuwa ni jambo la kawaida kwa watu wanaozungumza lugha au anuwai ya lugha yoyote ile kama tulivyoonyesha na mifano ya hapo juu.

Kimo cha vokali kinaweza kutokana pia na usimilisho ambapo hutokea udondoshaji wa irabu ya kwanza na ile ya pili ikaongeza sifa za kimo ili kufidia ule udondoshaji kwa mfano.

ma + inu - Miinu

wingi jino neno

Wakati mwingine irabu huungana katika mipaka ya mofimu

/li/ + /isimbwa/ - /li:simbwa/

ya umbwa ya umbwa

Kimo cha vokali chaweza pia kutokana na njeo kwa mfano

/atsiri/ - alienda

/atsiiri/ - ameenda

## 2.4 KIBUKUSU

Lahaja yaKibukusu ina jumla ya fonimu 25, 20 zikiwa ni fonimu konsonanti na 5 zikiwa ni fonimu irabu kama inavyoonyesha katika jedwali ifuatayo

| | midomo | midomo meno | ufizi | Kaakaa ufizi | kaakaa | Glota |
|---|---|---|---|---|---|---|
| vizuiwa | p | | t | | | k |
| nazali | m | | n | | ɲ | ŋ |

| | midomo | midomo meno | ufizi | kaakaa ufizi | kaakaa | Glota |
|---|---|---|---|---|---|---|
| vikwamizwa | β | f | s | | | x |
| Vizuiwa kwamizwa | | | | tʃ | | |
| kimandende | | | r | | | |
| kitambaza | | | l | | | |
| viyeyushi | w | | | | j | |
| Sauti mlolongo | m b | | nd | ɲɟ | | ŋg |

1) /t/ katika litala (boma la ng'ombe)

tasa (ongeza)

2) /m/ katika kumukhono (mukono)

kumunina (mlima)

3) /n/ katika Omukhana (msichana)

kamanani (majani)

4) /b/ katika bacha (hepa)

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | bulo (mtama) |
| 5) | /s/ | katika | sala (omba) |
| | | | subila (amini) |
| 6) | /x/ | katika | khacha (ulafi) |
| | | | khenga (chonga) |
| 7) | /tʃ/ | katika | cha (enda) |
| | | | bocha (kula kama kuku) |
| 8) | /ŋ/ | katika | ng'enga |
| | | | Khung'ona (tengeneza) |
| 9) | /ɲ/ | katika | kumunywanywa (fujo) |
| 10) | /f/ | katika | fwala (vaa) |
| | | | funa (vunja) |
| 11) | /r/ | katika | rura (toka) |
| | | | rera (leta) |
| 12) | /l/ | katika | olile (umekula) |
| | | | lila (lia) |
| 13) | /p/ | katika | khulipa |
| 14) | /k/ | katika | kumwima (amini) |
| | | | kamaani (nguvu) |
| 15) | /w/ | katika | wecha (ulikuja) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | khukwa (anguka) |
| 16) | /mb/ | katika | kamaomba (mawele) |
| | | | embeo (baridi) |
| 17) | /nd/ | Katika | enda (tumbo) |
| | | | linda (ngoja) |
| 18) | /ŋg/ | katika | engala (kitu cha mvirinyo) |
| 19) | /ɲdʒ/ | katika | enjala (njala) |
| | | | enjome (chombo cha kuvulia samaki) |
| 20) | /j/ | katika | yaya (mtu wa ukoo) |
| | | | yeya (fagia) |

## Vokali

Vokali za Kibukusu ni kama zifuatazo:



1) /a/ katika mala (maliza)

mila (meza)

2) /ɛ/ katika beka (nyoa)

Bea (danganya)

3) /I/ katika lila (lia)

Yira (na)

4) /ɔ/ katika Bola (oza)

loba (vua)

5) / u/ katika kula (nunua)

nuna (nyanya)

Kama katika lahaja za kilogooli na kiisukha, lahaja ya kibukusu pia ina irabu ndefu. Kwa mfano.

1) mala - /mala/ - kumaliza

maala - /ma:la/ - kukoroga

2) βeka - /ɓeka/ - Nyoa nywele

βeeka - /ɓe:ka/ wanajifunza

3) lila - /lila/ - lia

liila - /li:la/ - kula ukitumia

4) βola - /βɔla/ - Oza

βoola - /βɔ:la/ - Ongea

5) Khula - /Xula / - kua

Khula - /Xu: la/ - ng'oa

**2.5 KIKISA**

Idadi ya fonimu katika lahaja ya Kikisa ni 29. Fonimu konsomunti ni 24 nazo fonimu irabu ni tano

Jedwali ifuatayo inaonyesha fonimu konsonanti za kisa

| | Midomo | Midomo meno | Ufizi | Kaakea | Kaakea ufizi | Kaakea lami | Glota |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |

| | Midomo | Midomo meno | Ufizi | Kaakaa | Kaakaa ufizi | Kaakaa laini | Glota. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kipasuo | P | | t | | | k | |
| Nazali | M | | n | ɲ | | ŋ | |
| Kitambaza | | | | l | | | |
| | | | r | | | | |
| Kikwamizwa | β | f | s | j | s ʃ | | h x |
| Kuzuiwa kwamizwa | | | | | | | |
| Kufululizwa huru | | | | | | w | |
| Mlolongo | mb | nd nz | | ɲdʒ | | ŋg | |
| | | | | | | | |

Fonimu konsonanti za Kikisa zilizoorodheshwa

1. / l / katika loma(sema)

langa(ita)

| | | |
|---|---|---|
| 2. /f/ | katika | fuka(songa ugali) |
| | | fisa (ficha) |
| 3. /r/ | katika | raanga(chokoza) |
| | | ira (peleka) |
| 4. /m/ | katika | fuma(sifika) |
| | | khuuma (paza sauti) |
| 5. /k/ | katika | kaama (twaa) |
| | | laka (ahichi) |
| 6. /β/ | katika | βola(oza) |
| | | βaamba (sulubishi) |
| 7. /s/ | katika | saamba (choma kwa moto) |
| | | fisa (ficha) |
| 8. /ʃ/ | katika | shuula (pindua) |
| | | ishiria (laana) |

| | | |
|---|---|---|
| 9. /ŋ/ | katika | ling'ondo (peni) |
| | | tsing'ombe (ng'ombe) |
| 10. /ɲ/ | katika | okhuunya (via) |
| | | khonya (saidia) |
| 11. /n/ | katika | kaania (kataza) |
| | | okhununa |
| 12. /p/ | katika | khupa (piga) |
| | | lipusi (paka) |
| 13. /t/ | katika | kaatia (danganya) |
| | | eshititi (kidogo) |
| 14. /w/ | katika | waayo (toka hapa) |
| | | okhweya (fagia) |
| 15. /x/ | katika | khomba (ramba) |
| | | khama (potea) |
| 16. /j/ | katika | yuka (tembea haraka) |

| | | |
|---|---|---|
| | | rayo (weka hapa) |
| 17. /ts/ | katika | itsa (njoo) |
| | | matsai (damu) |
| 18. /nd/ | katika | kaanda (duwaa) |
| | | khuchenda (kutembea) |
| 19. /ng/ | katika | langa (ita) |
| | | ranga (anzisha) |
| 20. /nz/ | katika | inzala (njaa) |
| | | inzokha (nyoka) |
| 21. /ḿb/ | katika | imbala (alama) |
| | | kaamba (hubiri) |
| 22. /ʧ/ | katika | choma (penda) |
| | | chaka (anza) |
| 23. /h/ | katika | ahambi (karibu) |
| | | lihe( vita |
| 24 /ʤ / | katika | injira (njia) |
| | | ebinji (vingi) |

Ni muhimu kusisitiza kuwa katika lahaja za Kiisukha, Kilogooli na Kikisa idadi ya fonimu konsonanti ni ishirini na nne ambayo ni idadi inayoafikiana na fonimu-konsonanti zilizoorodheshwa na Itebete (1974) kuwa zilichaguliwa na wamisheni

kuwa alfabeti ya lugha sanifu ya Kiluyha ambayo ingetumiwa katika maandishi, ingawaje Itebete hakuonyesha mbinu iliyotumika kuzihamisha fonimu –konsonanti hizi.

## VOKALI

Lahaja yaKikisa ina idadi ya fonimu-irabu tano kama inavyoonyeshwa katika jedwali ifuatayo.



Maneno yafuatayo yanatudhihirishia fonimu irabu za kisa

| | | |
|---|---|---|
| 1. /a/ | katika | kana (hadithia) |
| | | yaba (chimba) |
| 2. /e/ | katika | mera (mea) |
| | | rera (lea) |
| 3. /β/ | katika | bola (oza) |
| | | loba (kataa) |

| | | |
|---|---|---|
| 4. /i/ | katika | mira (meza) |
| | | ira (peleka) |
| 5. /u/ | katika | fuma (sifika) |
| | | kuka (babu) |

Orodha hii ya Irabu za Kikisa inafanana na orodha ya Irabu za Kiluyia iliyoafikiwa na wamisheni waliokuwa wakijaribu kuisahihisha lugha hii ili kuibua lugha ambayo ingetumika katika uandishi na usambazaji wa injili ya Kristo Itebete(1974) ameziorodhesha hiziIrabu tano zilizoafikiwa kuwa ni a, e,iI, o, u.

Irabu zote tano zilizoorodheshwa hapo juu zinachukua sifa ya urefu katika silabi za baadhi ya maneno. Aidha sifa hii ya urefu katika Irabu za Kikisa inasababisha tofauti ya maana katika jozi ya maneno.Aidha sifa hii ya urefu katika Irabu za kisa inasababisha tofauti ya maana katika jozi ya maneno .

Tazama mifano ifuatayo

| | | | |
|---|---|---|---|
| (1) | bira - | /β i r a / - | chemka |
| | biira- | /β iː r a / - | ambia |

(2) kana- /k a n a/ -hadithia

/k a :n a/ -kataa

(3) bola- /βɔl a / -oza

/βɔ :l a/ -sema

(4) rera- /r e r a/ -lea

/ r e : r a/ -leta

(5) rula- /r u l a/ -toka

ruula /r u: l a/ -twa mzigo

Mengi kuhusu sauti hizi yatajadiliwa katika moja wapo ya sura ya kazi hii.

# SURA YA TATU

## TOFAUTI ZA KILEKSIKA.

Ili kuweza kubainisha tofauti za kileksika miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja hizi nne, yaani Kilogooli, Kibukusu, Kikisa na Kiisukua, tutatumia mbinu ya takwimu leksika .Hii ni mbinu ya kuchunguza na kutumia takwimu za msamiati wa lugha mbili au zaidi ili kuweza kuona ni kwa kiasi gani zinasikilizana [TUKI (1990)]. Hapo mwanzoni mbinu hii iliendelezwa pamoja na ile ya glotokronolojia kileksika katika kujaribu kuchunguza uhusiano wa kifamilia katika lugha [TUKI (1990)], ili kuweza kubainisha uhusiano uliopo baina ya lugha zilizotokana na lugha zazi moja katika isimu historia.

Hata hivyo matumizi ya takwimu leksika hayabanwi katika mipaka ya isimu historia pekee,bali twaweza kutumia takwimu leksika ili kuweza kubainisha mahusiano ya kiisimu bila kuzingatia maswala ya kihistoria .

Kwa kutumia mbinu hii ya takwimu kileksika ,tumeorodhesha maneno mia mbili katika lugha ya kiswahili ,kisha tukayatafsiri maneno hayo hadi katika lahaja tunazo zishughulikia .Katika kuorodhesha maneno hayo tumezingatia maoni ya wasomi ambao wamewahi kujishughulisha na takwimu leksika [Gudchinsky(1956&1964)],Swadesh(1955),Cole(1967),Samarin(1967),Lehmann (1973), na Bynon (1977).Kulingana na wasomi hawa ,orodha kama hizi za kulinganisha msamiati,zapaswa kuhusisha maneno yanayozingatiwa na wazungumuzaji wa lugha au lahaja fulani kuwa ni ya kimsingi.Kwa mujibu wao ,msamiati huu hudumishwa na wazungumzaji wa lugha au lahaja fulani kwa muda mrefu bila kubadilika.Vilevile ,kina cha kupoteza msamiati wa kimsingi huwa ni sawa katika lugha au lahaja zote .Hali kadhalika msamiati huo hujishughulisha na tajribia za binadamu zilizoko bila kujali utamaduni wa wazungumzaji na hujumuisha maneno kama vile yale ya sehemu za mwili ,mifanyiko ya kibayolojia kama vile kuzaa ,maumbile ya kijiografia ,mahusiano ya kijumla yanayowakilishwa na viwakilishi ,vionyeshi,ukanushi,ukubwa au udogo wa vitu na nambari moja hadi tisa.

Kwa kuzingatia hayo yote tumeweza kuorodhesha maneno yafuatayo:

(ORODHA YA MANENO)

| | KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU | KIKISA | KIISUKHA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kwenda | Geenda | Kenda | Okhuchenda | Chenda |
| 2 | Meza | Mila | Mila | Okhumira | Mila |
| 3 | Shika | Gumila | Tila | Okhutila | Kumila(chimi la) |
| 4 | Ona | Lola | Bona | Okhulola | Lola |
| 5 | Sikia | Hulla | Ulila | Okhulira | Hulila |
| 6 | Imba | yiimba | Khukwimba | Okhwimba | Yimba |
| 7 | Nyonya | Nuuna | Nuna | Okhununa | Nuna |
| 8 | Kula | Nyaanya | Lya | Okhulia | Lya |
| 9 | iga | Hula | Khupa | Okhutuya | Rumula |
| 10 | Enda | Zia | Cha | Okhutsia | Tsia |
| 11 | Kimbia | Nyagula | Tima | Okhwirukha | Khwirukhaka |
| 12 | Vunja | Vunenyia | Funa | Okhufunaka | Meneka |
| 13 | Kuna | Yaga | Yaikala | Okhuwiyeka | Yeka |
| 14 | Osha | Kwogidza | Singa | Okhuwosia | Singa\Yokits a |
| 15 | Kuja | Hamba | Yicha/ Icha | Okhwitsa | Hamba/ Itsa |
| 16 | Jaribu | Geridza | Kheka | Okhutema | Chelitsa |
| 17 | Omba/ Sali | Saala | Saba/ Sala | Okhusaya | Saala |

| | KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU | KIKISA | KIISUKHA |
|---|---|---|---|---|---|
| 18 | Vua | Luba | Loba | Okhuloba | Luba |
| 19 | Kua (umri) | Viruka | Khukhule | Okhukhula | Tukha |
| 20 | Panda (mmea) | Taaga | Biala | Okhuraka | Raka |
| 21 | Tengeneza (umba) | Loomba | Khung'ona | Okhukasia | Lomba |
| 22 | Anguka | Gua | Khukwa | Okhukwa | Lomoloma |
| 23 | Fanya kazi | Yinzila | Khola | Emilimo | Khuinzila |
| 24 | Pika | Deeka | Tekha | Okhutekha | Tekha |
| 25 | Zungumza | Moloma | Losia/ Kachula | Okhuboola | Lomoloma |
| 26 | Laani | Laama | Himaa | Okhulama | Laama |
| 27 | Leta | Leeta | Khurera | Okhurera | Leera |
| 28 | Fagia | Yeya | Yeya | Okhweya | Yenza |
| 29 | Ongeza | Meeda | Tasa | Okhumeta | Tesa |
| 30 | Kunywa | Nywa | Nywa | OKhunywa | Ng'wa |
| 31 | Hesabu | Baliza | Bala | Okhubasia | Balitsa |
| 32 | Ngoja | Liinda | Liinda | Okhulinda | Linda |
| 33 | Ua | Yita | Yira | Okhuira | Yira |
| 34 | Zaa | Kwivula | Khiluba | Okhwibula | Khwibula |
| 35 | Anza | taanga | Yanja | Okhuchaka | Ranga |

| | KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU | KIKISA | KIISUKHA |
|---|---|---|---|---|---|
| 36 | Pea | Haana | Aane | Okhwesia | Haana |
| 37 | Puruka | Buruka | Purukha | Okhupulukha | Pulukha |
| 38 | Nunua | Gura | Kula | Okhukula | Kula |
| 39 | Iba | Yiba | Yiiba | Okhwiba | Huba |
| 40 | Danganya | Beha | Bea | Okhukatia | Khukata |
| 41 | Lima | Lima | Lima/ Yaba | Okhulikma | Lima |
| 42 | Cheza | Kina | Inyaa | Okhubaya | Baya |
| 43 | Vuna | Gesa | Kea | Okhufuna | Chesa/ Buna |
| 44 | Leta | Leda | Lera | Okhulera | Leera |
| 45 | Fagia | Yeeya | Yeya | Okhweya | Yenza |
| 46 | Simama | Singila | Tima | Okhusinjira | Sinjila |
| 47 | Ongeza | Meeda | Tasa | Okhumeta | Tesa |
| 48 | _zuri | _lahi | _layi | Obulayi | _lahi |
| 49 | _baya | _damanu | _pii | Obubi | _pi |
| 50 | Konda | Uvungafu | _nyelele | Okhutora | _ngahu/ Nyelele |
| 51 | _eusi | _mwamu | BNumali | Obumali | _mwamu |
| 52 | _eupe | _lavu | Buanga | Obulaffu | _labu |
| 53 | _ekundu | Uviwakonyu | Bukesene | Obwakhanyo | _muchi |
| 54 | Baridi | Uvuzillu | Bunyifu | Obushindu | Bushindu |

| | KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU | KIKISA | KISUKHA |
|---|---|---|---|---|---|
| 55 | Moto | Uvushi | Bubile | Olluya | Mulilu |
| 56 | Urefu | Uvutambi | Buleyi | Oburambi | Burambi |
| 57 | Fupi | Uvwimbi | Bubimbi | Obiwimbichiti | Vwimbi |
| 58 | Mbali | Ihale | Atayi/ Aleyi | Ekhale | Ihale |
| 59 | Karibu | Ahimbi | Aembi | Ahambi | Himbi |
| | | | | | |
| 60 | Haraka | Vwangu | Bwangu | Tsimbiro | Bwangu |
| 61 | Moja | Killa | Ndala | Shilala | Shilala |
| 62 | Polepole | Ghalaha | Kalahaa | Kaala | Kalaha |
| 63 | Yai | Ilivuyu | Likii | Libuyu | Libuyu |
| 64 | Kazi | Igasi | Kimilimo | Emilimo | Milimu/ Ikasi |
| 65 | Kifo | Ilikuza | Lifwa | Okhufwa | Likhutsa |
| 66 | Ndizi | Amagomiya | Litore/ Lirofu | Amaramwa | Maremwa/ Mengu |
| 67 | Uwanja | Ikiguti | Sikuri | Eshikuri | Shikuri |
| 68 | Jua | | Kumumu | Eshitere | Mbasu |
| 69 | Mvua | Imbula | Efula | Ifula | Imbula |
| 70 | Mwezi | Umweli | Kumwesi | Omwesi | Mweli |
| 71 | Jua | Umbasu | Kumumu | Eliuba | Lyuba |
| 72 | Dunia | Ikabala | Sibala | Eshialo | Shibala |

| | KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU | KIKISA | KIISUKHA |
|---|---|---|---|---|---|
| 73 | Nyota | Ing'ereng'ani | Engeriesi'g | Ingi'irin'gini | Ingi'inig'ini |
| 74 | Siku | Lidiku | Endalo | Tsinyanga | Litukhu/ Inyanga |
| 75 | Mzizi | Umuli | Lusia/ Kumuli | Omusi | Muli |
| 76 | Nyasi | Uvunysi | Lunyasi | Obulimo | Bunyasi/ Busese |
| 77 | Mbegu | Embego | Lumicho | Obufuwa | Bukuhtsa |
| 78 | Mto | Umugera | Luluchi | Omwalo | Muchela |
| 79 | Maji | Amadzi | Kamechi | Amatsi | Matsi |
| 80 | Ziwa | Inyaanza | Enyanya | Olukose | Inyanza/ Lubele |
| 81 | Mawingu | Amagesi | Lifumbi | Lilesi | Malesi |
| 82 | Upepo | Imbuza | Luucho | Simbalakusi | Muyeka |
| 83 | Mifugo | Ibitugo | Chikhafu | Singombe | Miruko |
| 84 | Kondoo | Ligondi | Likhafu | Amatsai | Musai |
| 85 | Mkia | Umukila | Kumukhinga | Omushira | Mshila |
| 86 | Kuku | Engoko | Engokho | Ingokho | Ingokho |
| 87 | Mbuzi | Imbuli | Embusi | Imbusi | Imbuli |
| 88 | Fahali | Igiriki | Eunwa | Ichurushi | Ichilishi |
| 89 | Paka | Ikibaga | Epusi | Lipusi | Lipusi/ aka |

| | KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU | KIKISA | KIISUKHA |
|---|---|---|---|---|---|
| 90 | Mbwa | Imbwa | Embwa | Imbwa | Isimbwa |
| 91 | Sungura | Ikefwoyo | Enduyu | Eshituyu | Eshihungula |
| 92 | Nyoka | Inzoka | Endemu | Iknzokha | Inzukha |
| 93 | Kobe | Likudu | Lichutu | Likhutu | Likhutu |
| 94 | Ndege/Nyuni | Linyonyi | Enyonyi | Linyonyi | Linyonyi |
| 95 | Nzi | inzi | Esi | Isi | Inji |
| 96 | Samaki | Isuzi | Eng'eni | Inyeni | Isutse |
| 97 | Manyoya/ Mabawa | Liraha | Lifungo | Libaa | Mabaha |
| 98 | Machozi | Amaliga | Kamasika | Amasika | Milika |
| 99 | Maziwa | Amavere | Kamabele | Amabere | Mabele |
| | | | | | |
| 101 | Pembe | Ulwiga | Lulwika | Olwika | Lwika |
| 102 | Kiti | Endebe | Sisala | Eshifumbi | Shisako/ Shirumbi |
| 103 | Chungu/Nyungu | Inyingu | Eningilo | Eshirabu | Inyungu/ Isiongo |
| 104 | Nyumba | Inyumba | Enju | Inzu | Inzu |
| 105 | Usaa | Amahira | Kamahila | Amafira | Mahila |
| | | | | | |
| 106 | Mtu | Umundu | Omuntu | Omundu | Mundu |

| | KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU | KIISA | KIISUKHA |
|---|---|---|---|---|---|
| 107 | Mwanamume | Umusadza | Umusiecha | Omusatsa | Mutsatsa |
| 108 | Mwanamke | Omukali | Omukhesi | Omukhesi | Mukhali,<br>Mukhokho |
| 109 | Mvulana | Omuyaayi | Omusoleli | Omusiani | Muyayi |
| 110 | Msichana | Omukaana | Omukhana | Omukhana | Mukhana |
| 111 | Mtoto | Umwana | Omwana | Omwana | Mwana |
| 112 | Babu | Guga | Guka | Guka | Guka |
| 113 | Nyanya | Guuku | Kukhu | Kukhu | Kukhu |
| 114 | Mama | Maama | Mayi | Maama | Mama |
| 115 | Mjomba | Kooza | Khoocha | Khosa | Khosa |
| 116 | Kichwa | Umutwi | Kumurwe | Omurwi | Murwi |
| 117 | Mkono | Umukono | Kmukhonoa | Omukhono | Mukhono |
| 118 | Shingo | Ligoti | Likosi | Likosi | Ling'ori |
| 119 | Bega | Amavega | Libeka | Libeka | Libeka |
| 120 | Mguu | Ekerenge | Sikele | Eshirenje | Shilenje |
| 121 | Kidole | Ekedete | Lulwala | Eshitere | Shitere |
| 122 | Jicho | Emoni | Emoni | Imoni | Imoni |
| 123 | Sikio | Litu | Liruu | Eshiruwi | Shiroyi |
| 124 | Pua | Amulu | Liliolu | Eshiulu | Lyulu |
| 125 | Goti | Llu | Lisikamo | Lisikamo | Lisikamo |
| 126 | Kumbo | Inguka | Ekhumbo | Ikhumbo | Likhumbo |

| | KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU | KIKISA | KIISUKHA |
|---|---|---|---|---|---|
| 127 | Matako | Amadako | Kamatakho | Amatakho | Matakho |
| 128 | Sura | Mmoni | Mumoni | Mmoni | Likondo |
| 129 | Ini | Ingudumani | Sinii | | Ingurumani |
| 130 | Figo | Idzimbigo | Embiko | Ifuko | Imbiko |
| 131 | Ubavu | Inzimbalu | Lubafu | Olubafu | Lubafu |
| 132 | Mdomo | Umunwa | Kumunwa | Omunwa | Munwa |
| 133 | Nywele | Llisu | Lichune | Liswi | Liswi |
| 134 | Titi | Ulebere | Lituru | Olubere | Lubere |
| 135 | Jino | Llino | Lilimo | Elino | Lino |
| 136 | Ulimi | Ullimi | Lulimi | Olulimi | Lulimi |
| 137 | Kidevu | Ikinanwa | Silefu | Eshimumu | Shitefu |
| 138 | Usiku | Uvudiku | Sillo | Eshiro | Butukhu |
| 139 | Radi | Uluheni | Lueni | Olweni | Luheni |
| 140 | Mlima | Ikiguru | Sikulu | Eshikulu | Shikulu |
| 141 | Moshi | Umuochi | Lilisi | Omwasi | Lyoshi |
| 142 | Moto | Umullu | Kumulilo | Omuliro | Mulilu |
| | | | | | |
| 143 | Jiwe | Ligina | Libale | Lichina | Lichina |
| 144 | Kamba | Umugoye | Kumukoye | Omukoye | Mukoye |
| 145 | Barabara | Inzila | Ngila | Omuanda | Muhanda |
| 146 | Kitu | Ikindu | Sindu | Eshindu | Shindu |

| | KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU | KIIKISA | KIISUKHA |
|---|---|---|---|---|---|
| 147 | Zawadi | Ikihanwa | Sianwa | Eshianwa | Shihanwa |
| 148 | Udongo | Uvudohi | Kamatosi | Amatoyi | Litoyi |
| 149 | Jivu | Ligoke | Likokhe | Likoshe | Likoshe |
| 150 | Mchanga | Umuyeke | Kumuyekhe | Oluyeshe | Muyeshe |
| 151 | Vumbi | Uluguki | Lufumbi | Olufu | Lukushi |
| 152 | Kisu | Umbano | Kubano | Ombano | Llitwa/Mmba nu |
| 153 | Mkuki | Litimu | Lifumo | Lifumo | Lirimu |
| 154 | Shoka | Imbazi | Eaywa | Imbatsi | Ihaywa |
| 155 | Nzige | Isige | Chisike | Litete | Isichi |
| 156 | Kifagio | Ichieyo | Siyeywe | Eshieyo | Shyeyo |
| 157 | Chifu | Umwami | Omwami | Omwami | Mukhongo |
| 158 | Mkulima | Umulimi | Omulimi | Omulimi | Mulimi |
| 159 | Mwizi | Umwivi | Omwifwi | Omwifi | Shihubi |
| 160 | Kivuli | Ikilili | Sinini | Eshinini | Shinini |
| 161 | Msitu | Umulitu | Kumusiru | Omutsuru | Muliru |
| 162 | Mvuvi | Umuluvi | Omulobi | Omulobi | Muluvi |
| 163 | Mti | Umusala | Kumurongor o | Omusala | Musala |
| 164 | Tawi | Litu | Lisafu | Lisafu | Liru/Lisambu |
| 165 | Mingi | Ibinyingi | Bikali | Ebinji | Binyishi |

| | KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU | KIKISA | KIUUKHA |
|---|---|---|---|---|---|
| 166 | Kidogo | Ekekeke/ekedidi | Khationgo | Eshititi | Shiti(ti) |
| 167 | Kubwa | Ekenene | Kuakli | Obukali | Shikali |
| 168 | Mbili | Bibili | Chibili | Tsibili | Bibili |
| 169 | Tatu | Bibaga | Bitaru | Bitaru | Bibaka |
| 170 | Nne | Bine | Chinne | Binne | Binne |
| 171 | Sita | Siita | Sitaa | Bisasaba | Bisasaba |
| 172 | Kumi | Ilikumi | Likhumi | Ekhumi | Likhomi |
| 173 | Saba | Saba | Saba | Saba | Bisaba |
| 174 | Chache | Bidididi | Bikekhe | Bititi | Bichechi |
| 175 | Siku(Wingi) | Amadiku | Chindalo | Tsinyanga | Tsinyanga |
| 176 | Haraka | Idzimbilu | Khangu | Bwangu | Bwangu |
| 177 | Kukataa/Kutopenda | Okusuura | Khabiile | Okhuloba | Khwambakhana |
| 178 | Wanawake | Avakaaye | Balosi | Abakhasi | Bakoko |
| 179 | Kitanda | Ikidali | Sitali | Eshitanda | Shitali |
| 180 | Mfupa | Ikigumba | Sikumba | Eshikumba | Shikumba |
| 181 | Mnyama | Inyama | Esang'i | Isolo | Isolo |
| 182 | Mkundu | Emudako | Kumutwi | Omutwi | Bunero |
| 183 | Kidonda | Ligule | Likonjo | Likule | Likule |
| 184 | Ukuta | Lididji | Lisisi | Lisisi | Lisisi |

| | KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU | KIKISA | KIISUKHA |
|---|---|---|---|---|---|
| 185 | Sauti | Umwoyo | Kumumilo | Omwoyo | Mwoyo |
| 186 | Mwiba | Llifwa | Liwa | Liwa | Libwa |
| 187 | Miiko/Mwiko | Imiluka | Kumusilo | Tsishira | Muchira |
| 188 | Miwa | Umukonye | Kumwiba | Omukhonye | Mukhonye |
| 189 | Fuvu | Ikihanga | Sianga | Eshianganga | Shihanga |
| 190 | Kushiba | Kwiguta | Khukhwikura | Okhwikura | Khwikura |
| 191 | Kuapa | Kwisuha | Silulu | Okhwifuliba | Khwisuha |
| 192 | Tapika | Luka | Khurusia | Okhusala | Khusala |
| 193 | Uzito | Uvulitu | Busiro | Obusiro | Bulitoho |
| 194 | Ua | Ulugaga | Lumako | Olukaka | Lukaka |
| 195 | Ndama(Mwili) | Ulusaya | Lusaya | Indama | Luseya |
| 196 | Kucheka | Seka | Chekha | Okhusetkha | Khusekha |
| 197 | Nono | Kukomera | Khukhomera | Okhukhomer a | Khukhomera |
| 198 | Mkono | Umukono | Kumukhono | Omukhono | Mukhono |
| 199 | Ndevu | Idzindelu | Bunanwa | Tsindefu | Tsindelu |
| 200 | Mbavu | Idzimbalu | Tsimbafu | Tsimbafu | Tsimbalu |
| | | | | | |

Kutokana na orodha hii, tungependa kuthibitisha ya kwamba matatizo ya kuwasiliana

kimaongezi hutokea miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja hizi kutokana na sababu Zifuatazo:

a) Lahaja tofauti kutaja kitu kimoja kwa kutumia msamiati tofauti.
b) Maneno yanayotamkwa sawa na kukaribiana kimatamshi katika lahaja hizi hubeba maana tofauti.

a)Lahaja tofauti kutaja kitu kimoja kwa kutumia msamiati tofauti

kutokana na orodha yetu, tofauti zifuatazo za kisamiati zinapatikana.

i)Tofauti za kisamiati baina ya Kilogooli na Kibukusu .

| KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU |
|---|---|---|
| Ona | Lola | Bona |
| Kimbia | Nyagula | Tima |
| Jaribu | Geridza | Kheka |
| Kua | Viruka | Khukhuli |
| Panda(mmea) | Taaga | Biala |
| Zungumza | Moloma | Kachula |
| Cheza | Kina | Inyaa |
| Simama | Singila | Tima |
| -eusi | -mwamu | -mali |
| -eupe | -lavu | -wanga |

| | | |
|---|---|---|
| -ekundu | -vwakonyu | -beseme |
| Moto | Uvushu | Bubile |
| Ndefu | Uvutambi | Buleyi |
| Yai | Ilivuyu | Likii |

| **KISWAHILI** | **KILOGOOLI** | **KIBUKUSU** |
|---|---|---|
| Ndizi | Amagomiya | Litore |
| Dua | Umbasu | Kumumu |
| Siku | Ilidiku | Endalo |
| Mbegu | Embego | Lumicho |
| Mto | Umugera | Luluchi |
| Mawingu | Amalesi | Lifumbi |
| Kondoo | Iligondi | Likhere |
| Sungura | Ikefweyo | Enduyu |
| Nyoka | Inzoka | Endemu |
| Chungu | Inyingu | Eningilo |
| Mvulana | Omuyayi | Omusoleli |
| Shingo | Iligoti | Likosi |
| Mguu | Ekerenge | Sikele |
| Ini | Ingudumani | Sinii |
| Nywele | Lisa | Lichune |
| Titi | Ulubere | Lituru |

| KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU |
|---|---|---|
| Kidevu | Ikinanwa | Silefu |
| Usiku | Ikinanwa | Sillo |
| Moshi | Umuochi | Lilisi |
| Jiwe | Iligina | Libale |
| vumbi | Uluguki | Lufumbi |
| Mkuki | Ilitimu | lifumoea |

| | | |
|---|---|---|
| Shoka | Imbazi | Eaywa |
| Kivuli | Ikilili | Sinini |
| Mti | Umusala | Kumurongoro |
| Kubwa | Ekenene | Kubofu |
| Chache | Bodididi | Bikekhe |
| Wanawake | Avakaaye | Balosi |
| Mnyama | Inyama | Esayi |
| Kidonda | Iliguli | Likonjo |
| Tapika | Luka | Khurusia |
| Sauti | Umweyo | Kumumilo |
| Kuapa | Khwisuha | Silulu |

Tofauti za kimsamiati baina ya Kilogooli na Kibukusu.

| KISWAHILI | KILOGOOLI | KIBUKUSU |
|---|---|---|
| Shika | Gumila | Okhutila |
| Piga | Hula | Okhuituya |
| Kimbia | Nyagula | Okhwirulkha |
| Kua | Vivuka | Okhukhula |
| Tengeneza | Loomba | Okhukasia |
| Cheza | Kina | Okhubaya |
| Konda | Uvungafu | Okhutora |
| -eusi | -mwamu | -mali |
| Haraka | Vwangu | Tsimbira |
| Kazi | Igasi | Emilimo |
| Kifo | Likuza | Okhufwa |
| Dunia | kibala | Eshialo |
| Mbegu | Embegu | Obufwa |
| Mto | Umgera | Omwalo |
| Upepo | Imbuza | Simbalakusi |
| Sungura | Twekfwoyo | Enduyu |
| Samaki | Isuzi | Inyeni |
| Manyoya | Iliraha | Libaa |
| Kiti | Endeve | Esifumbi |
| Chungu | Inyingu | Eshirabu |

| Kiswahili | Kilogooli | Kibukusu |
|---|---|---|
| Mvulana | Umuyaayi | Omusiani |
| Shingo | Iligoti | Likosi |
| Kidevu | Ikinanwa | Eshimumu |
| Vumbi | Uluguki | Olufu |
| Msitu | Umulitu | Omutsuru |
| Tawi | Ilitu | Lisafu |
| Sita | Siita | Bisasaba |
| Kukataa | Okusuura | Okhuloba |
| Miiko | Imiluka | Tsishira |
| Kuapa | Khwisuha | Okhwifuliba |

Tofauti za msamiati baina ya Kilogooli na Kikisa

| **KISWAHILI** | **KILOGOOLI** | **KIKISA** |
|---|---|---|
| Kua | Viruka | Tukha |
| Cheza | Kina | Baya |
| Tapika | Juka | Khusala |
| -ekundu | Uvwakonyu | -muchi |
| Moto | -vushi | -hili |
| Mbegu | Embego | Bukutsa |
| Upepo | Imbuza | Muyeka |

| KISWAHILI | KILOGOOLI | KIKISA |
| --- | --- | --- |
| Sungura | Ikefwoyo | Shisungula |
| Sikio | Litu | Shiroyi |
| Kumbo | Inguka | Ikhumbi |
| Kivuli | Ikilili | Shinini |

Tofauti za msamiati baina ya Kibukusu na Kikisa.

| KISWAHILI | KIBUKUSU | KIKISA |
| --- | --- | --- |
| Ona | Bona | Okhulola |
| Kimba | Tima | Okhuwirukha |
| Jaribu | Kheka | Okhutema |
| Panda(mmea) | Biala | Okhuraka |
| Hesabu | Bala | Okhumbasia |
| Cheza | Inyaa | Okhubaya |
| Simama | Tima | Okhusinyira |
| Konda | Nyelele | Okhutora |
| -ekundu | Bubeseme | Obwakhanyu |
| Urefu | Buluyi | Oburambi |
| Mbali | Atayi/ Aleyi | Ekhale |
| Yai | Likii | Libuyu |

| KISWAHILI | KIBUKUSU | KIKISA |
|---|---|---|
| Ndizi | Lirofu | Amaramwa |
| Mbegu | Lumicho | Obufwa |
| Mto | Luluchi | Omwalo |
| Upepo | Luucho | Simbalakusi |
| Kondoo | Likhese | Likondi |
| Damu | Kamafuki | Amatsayi |
| Fahali | Eunwa | Ichulushi |
| Nyoka | Endemu | Inzokha |
| Manyoya | Lifumbo | Libaa |
| Chungu | Eningilo | Eshirabu |
| Mvulana | Omusoleli | Omusiana |
| Mguu | Sikele | Eshirenje |
| Kidole | Lulwala | Eshitere |
| Nywele | Lichune | Lifwi |
| Moshi | Lilisi | Omwesi |
| Jiwe | Liable | Lichina |
| Shoka | Eaywa | Imbatsi |
| Mti | Kumuronyoro | Omusala |
| Sita | Sita | Bisasaba |
| Kukataa | Khabiile | Okhuloba |
| Mnyama | Esayi | Isolo |
| Kidonda | Likoknjo | Likule |

| | | |
|---|---|---|
| Ua | Lumako | Lukaka |

Tofauti za masmiati baina ya Kibukusu na Kiisukha

| **KISWAHILI** | **KIBUKUSU** | **KIISUKHA** |
|---|---|---|
| Ona | Bona | Lola |
| Kimbia | Tima | Ilukhaka |
| Jaribu | Kheka | Chelitsa |
| Kuwa | Khukhale | Tukua |
| Panda(mmea) | Biala | Raka |
| Shida | Inyaa | Baya |
| _eusi | Bumali | _mwamu |
| _eupe | Buanga | _labu |
| _ekundu | Bubeseme | _muchi |
| Urefu | Bulei | Burambi |
| Mbali | Atayi | Ihale |
| Yai | Likii | Libuyu |
| Ndizi | Lirofu | Liremwa |
| Mbegu | Lumicho | Bukutsa |
| Mto | Luluchi | Muchela |
| Upepo | Luucho | Muyega |
| Sungura | Enduyu | Shisungula |

| | | |
|---|---|---|
| Nyoka | Endemu | Inzukha |
| Samaki | Eng'eni | Isutse |
| Manyoya | Lifumbo | Libaha |
| Chungu | Eningilo | Inyungu/ isiongo |
| Mvulana | Emusoleli | Muyayi |
| Mguu | Sikele | Shilenje |
| Ini | Sinii | Ingurumani |
| Nywele | Lichune | Liswi |
| Titi | Lituru | Lubele |
| Usiku | Sillo | Butuku |
| Moshi | Liliso | Lioshi |
| Jiwe | Libale | Lichina |
| Mti | Kumurongoro | Musala |
| Sita | Siita | Bisasaba |
| Saba | Saba | Bisambu |
| **KISWAHILI** | **KIBUKUSU** | **KIISUKHA** |
| Kataa | Khabiile | Khambakhane |
| Mnyama | Esang'i | Isolo |
| Kidonda | Likonjo | Likule |
| Uzito | Busiro | Bulitoho |
| Ua | Lumako | Lukaka |

Tofauti za msamiati baina ya Kikisa na Kiisukha

| KISWAHILI | KIKISA | KIISUKHA |
|---|---|---|
| Kua (umri) | Okhukhula | Tukha |
| Ueusi | Obumali | Bumwamu |
| Uekundu | Obwakhanyu | Bumuchi |
| Kifo | Okhufwa | Likhutsa |
| Mbegu | Obufwa | Bukutsa |
| Mto | Omwalo | Muchela |
| Sungura | Eshituyu | Shisungula |
| Chungu | Eshirabu | Inyungu |
| Figo | Ifuko | Imbiko |
| Kidevu | Eshimumu | Shirefu |
| Usiku | Eshiro | Burukhu |
| Vumbi | Olufu | Lukushi |
| Msitu | Omutsuru | Muliru |
| Mwiko | Tsishira | Muchiro |
| uzito | Obusiru | Bulitoho |

Kwa ujumla twaweza kusema kuwa tofauti hizi za kimsamiati hutatiza mawasiliano. Watu wanaozungumza lahaja hizi wanapowasiliana, kwani upande mmoja unaowasiliana huuliza maswali hapa na pale ili uweze kuelezewa maana ya maneno yasioeleweka katika lahaja inayohusika. Hata hivyo ni muhimu kusisitiza kwamba tofauti hizi za kileksika sio za kiwango kimoja na hutegemea wazungumzaji wa lahaja zinazohusika katika mawasiliano.

Ili kuweza kukadiria tofauti hizi, uchanganuzi wa kileksika unaweza kufanywa kwa kutumia mbinu ya kutafuta asilimia ya maneno nasaba baina ya lahaja mbili (cognate percentages). Hii ni mbinu iliyotumiwa na Gudchinskina Williams(1973). Hesabu inayotumika kupata asilimia hizi ni kama ifuatayo.

| | | |
|---|---|---|
| Asilimia ya maneno nasaba | | <u>idadi ya maneno nasaba x100</u> |
| Baina ya lahaja mbili | = | idadi yote ya maneno |
| (cognate percentage) | | yaliyoorodheshwa |

kwa kufuata njia hii, tunaweza kusema kuwa:

1) Idadi yote ya maneno yaliyoorodheshwa ni maneno 200
2) Ili kupata idadi ya maneno nasaba, tutachukuwa maneno yanayotofautiana baina ya lahaja mbili na tuondoe kutoka kwa mia mbili.

Kwa hivyo asilimia ya maneno nasaba baina ya lahaja tunazozingatia nkama ifujatayo.

Baina ya Kilogooli na Kibukusu $\frac{(200-51) \times 100}{200} = \frac{149 \times 100}{200}$

$=74.5\%$

Baina ya Kilogooli na Kikisa $\frac{(200-30) \times 100}{200} = \frac{170 \times 100}{200}$

$= 85\%$

Baina ya Kilogooli na Kiisukha $\frac{(200-12) \times 100}{200} = \frac{188 \times 100}{200}$

$=94\%$

Baina ya Kibukusu na Kikisa $\frac{(200-35) \times 100}{200} = \frac{165 \times 100}{200}$

$$=82.5\%$$

Baina ya Kibukusu na Kiisukha $\frac{(200-37)x100}{200} = \frac{163x100}{200}$

$$=81.5\%$$

Baina ya Kikisa na Kiisukha $\frac{(200-15)x100}{200} = \frac{185x100}{200}$

$$=92.5\%$$

Habari hii inawezwa kuwasilishwa katika jedwali kama ifuatavyo:

| | Kibukusu | Kiisukha | Kikisa | Kilogooli |
|---|---|---|---|---|
| Kibukusu | - | 81.5 | 82.5 | 74.5 |
| Kiisukha | 81.5 | - | 92.5 | 94 |
| Kikisa | 82.5 | 92.5 | - | 85 |
| Kilogooli | 74.5 | 94 | 85 | - |

Asilimia ya maneno nasaba miongoni mwa lahaja za Kibukusu,Kiisukha,Kikisa na Kilogoli.

Kutokana na hesabu yetu,tunapata kuwa shida nyingi zitatokea wakati watu wanaongea lahaja ya Kibukusu na Kilogooli wanapowasiliana kwani katika misamiati yao ya kimsingi maneno mengi hayalingani.

Kwa upande mwingine ,matatizo ya kimawasiliano ni machache wakati Waisukha na Walogooli wanapowasiliana kwani asilimia kubwa ya msamiati wao ya kimsingi inalingana.

Vilevile tunawezakusema kuwa ,hata ingawa kuna matatizo ya kimawasiliano ,watu wa lahaja hizi wanapowasiliana ,bado kuna uwezekano mzuri wa wao kuelewana kwa vile asilimia ya maneno nasaba ni ya juu na wala sio ya chini.

Vile vile ,kuna baadhi ya maneno ambayo hutamkwa sawa au kukaribiana kimatamshi na maneno ya lahaja nyingine ,lakini yakabeba maana tofauti kabisa.Kwa mfano maneno yafuatayo huamkwa kwa njia sawa au hukaribiana kimatamshi katika lahaja za Kilogooli na Kibukusu lakini yana maana tofauti.

| | KILOGOOLI | KIBUKUSU |
|---|---|---|
| Neno | Ilinyoni | linyoni |
| Maana | Ndege | Magugu |

| | KILOGOOLI | KIBUKUSU. |
|---|---|---|
| Neno | Uvutambi | Butambi |
| Maana | Urefu | Umaskini |
| Neno | Taga | Yaka |
| Maana | Kukuna | Kulima |
| Neno | Kwogidza | Khwokisa |
| Maana | kuosha | Makali |

Hali kama hii hupatikana katika lahaja zile zingine kama inavyojitokeza katika miano hii;

Mifano kutokana na na lahaja za Kibukusu na Kiisukha.

| | KIBUKUSU | KISUKHA |
|---|---|---|
| Neno | Imbula | Imbula |
| Maana | Mchuzi wa nyuki | Mvua |
| Neno | Simwamu | Shimwamu |
| Maana | Wasiwasi | Cheusi |
| Neno | Mela | Mela |

| | KIBUKUSU | KIISUKHA |
|---|---|---|
| Maana | Kulewa | Kukua(mimea) |
| Neno | Bisambu | Bisambu |
| Maana | Vichaka | Saba |
| Neno | Khukhuba | Khuhuba |
| Maana | Kuchanganyikiwa | Kuiba |
| Neno | Kamalesi | Malesi |
| Maana | Dawa | Mawingu |
| Neno | Shitere | shitere |
| Maana | Kucha | Kidole |
| Neno | Muliru | Muliru |
| Maana | Ndani ya sikio | Msitu |
| Neno | Lisamba | Lisambu |
| Maana | Shamba lisilolimwa | Tawi |
| Neno | Mchilo | Mchilo |
| Maana | Kwenda kabisa | Mwiko |

| | | |
|---|---|---|
| Neno | Kusakha | Khusekha |
| Maana | Kuomba wakati wa mavuno | Kucheka |

Mifano baina ya Kikisa na Kibukusu.

| | Kikisa | Kibukusu |
|---|---|---|
| Neno | Omusi | Kumusi |
| Maana | Mzizi | Mkundu |
| | | |
| Neno | Amasika | Amasika |
| Maana | Machozi ya kulia | Matanga |
| | | |
| Neno | Okhusaya | Khukhwisaya |
| Maana | Kuomba | ---------------- |

| | Kikisa | Kibukusu |
|---|---|---|
| Neno | Okhurora | Khulora |
| Maana | Kukonda | Loa maji |
| | | |
| Neno | Okhukasia | Khukasia |
| Maana | Kutengeneza | Kuvutia ~~(to woo)~~ |

| | | |
|---|---|---|
| Neno | Ifuko | Efukwo<br>fuko |
| Maana | Figo | |
| Neno | Olufu | Luufu<br>Siku tatu baada ya Sherehe za Kifo |
| Maana | Vumbi | |

Mifano baina ya Kilogooli na Kiisukha.

| | KILOGOOLI | KIISUKHA |
|---|---|---|
| Neno | Ikilili | swilili |
| Maana | Kivuli | Chomba cha muziki |
| Neno | Luka | Luka |
| Maana | Kutapika | Kwonga ugali |
| Neno | Ilifua | Iliibwa |
| Maana | mwiba | Kuisha |

Mifano baina ya Kikisa na Kiisukha.

| | KIKISA | KIISUKHA |
|---|---|---|
| Neno | Obusiru | Busiru |
| Maana | Uzito | Ujinga |
| Neno | Okhufwa | Khubwa |
| Maana | Kufa | Kuisha |
| Neno | Eshitere | Shitere |
| Maana | Siku | Kidole |
| Neno | Okhutora | Khutora |
| Maana | Kukonda | ororo |
| Neno | Okhurera | Khwera |
| Maana | kuleta | Kutaga yai |

Mifano kutoka Kilogooli na Kikisa

| | KILOGOOLI | KIKISA |
|---|---|---|
| Neno | Umusala | Omusala |
| Maana | Mti | Dawa |
| Neno | Umutwi | Omutwi |
| Maana | Kichwa | Mkundu |
| Neno | Ilifwa | Liwa |
| Maana | Mwiba | Kifo |
| Neno | Hamba | Hamba |
| Maana | Kuja | Kushika kuku ukitaka kuchinja |
| Neno | Indavu | Indabu |
| Maana | _eupe | nyungu |
| Neno | Ubusiro | obusiro |
| Maana | Ujinga | uzito |

Kwa ujumla twaweza kusema kuwa maneno ya aina hii hukanganya sana kwani kila kinachodhamiriwa na upande mmoja sicho kinachofasiriwa na upande mwingine wa mawasiliano. Hata Kama muktadha ambamo maneno haya yametamkwa unajulikana kwa pande zote mbili, bado kuna shida kwa vile upande mmoja wa mawasiliano hudhani kuwa ule mwingine umekosea kwa kutumia neno lisilofaa kutumika mahali lilipotumika.

Baada ya kushughulikia matatizo haya ya kileksika, hebu sasa tugeukie matatizo yanayotokana na tofauti mbalimbali za kifonetiki katika sura itakayofuata.

# SURA YA NNE

## UTATA UNAOTOKANA NA TOFAUTI ZA KIFONOLOJIA KATIKA LAHAJA

Katika sura hii tutajishughulisha na tofauti za kifonolojia miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja hizi nne yaani Kiisuka,KibukusuKilogooli na Kikisa.

Tutazingatia mifano ya miundo inayohusisha vipimo vya kifonologia katika viwango vya konsonanti na irabu yaani fonimu. Hata hivyo lazima tukumbuke kwamba kuna aina nyingine ya vipashio vya kifonolojia vinavyoh usisha sifa za kiarudhi kama vile kidatu,shadda,toni,urefu miongoni mwa mambo mengine.

Kulingana na W esterman na Ward(1970) Ladefoged e tal (1971),katika kila lugha na lahaja kuna baadhi ya sauti ambazo zina upekee wake katika lugha au lahaja nyingine na iwapo zitapatikana huwa katika mazingira tofauti.Hali hii ya kuwepo kwa tofauti katika sauti (fonimu) za lugha au lahaja imezaa matatizo hasa ya kimatamshi wakati watu wa lugha au lahaja tofauti wanapowasiliana kama tutakavyodhirisha kwa kutumia mifano kutoka lahaja hizi nne.

Tofauti za kimatamshi (kilafudhi) ni za aina mbili, yaani za (kilafudhi) kifonolojia na zile za kifonetiki (Roach, 1983). Wakati lafudhi za aina mbili zinapotofautiana kifonetiki

watu wa lugha au lahaja tofauti wanapowasiliana kama tutakavyodhirisha kwa kutumia mifano kutoka lahaja hizi nne.

Tofauti za kimatamshi (kilafudhi) ni za aina mbili, yaani za (kilafudhi) kifonolojia na zile za kifonetiki (Roach, 1983). Wakati lafudhi za aina mbili zinapotofautiana kifonetiki pekee yake, tunapata idadi sawa ya fonimu katika lafudhi zote lakini baadhi ya fonimu au fonimu zote hujitokeza kwa njia tofauti..

Kwa upande mwingine kuna tofauti za kifonolojia ambapo watu wanaozungumza lahaja(au lafudhi) fulani wana idadi tofauti ya fonimu na kwa hivyo mlinganuo kifonimu( phonetic contrast ) na wazungumzaji wa lahaja tofauti.

Ili kuweza kubainisha tofauti za sauti miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja hizi nne, tutazichanganua kwa kuzilinganisha sauti za hizo lahaja katika kiwango cha fonolojia vipande sauti ambazo huziona sauti za lugha kama ni mfuatano wa sehemu ndogondogo za vitamkwa. Ulinganishaji wa aina hii unaweza kutumika sio tu kuonyesha tofauti baina ya lugha au lahaja mbalimbali bali pia unaweza kutumika kutabiri matatizo ya kimatamshi yanayoweza kutokea miongoni mwa wazungumzaji wa lugha na lahaja husika.

Tukianza na lahaja ya Kilogooli, tunapata kuwa sauti /x/ ambayo ni kikwamizwa haipatikani kabisa katika lahaja hiyo. (Tazama jedwali ya hapo awali).

\Hata hivyo tunaona kuwa sauti hiyo inapatikana katika lahaja zinazosalia tatu, yaani kiisukha, kikisa na kibukusu. Jambo hili limefanya walogooli kupata shida kubwa sana wanapojaribu kutamka maneno katika lahaja hizo zingine tatu yaliyo na sauti /x/.

Badala ya kutumia sauti/x/ walogooli hutumia sauti /k/ ambayo ni sauti ya kipasuo mifano.

| KILOGOOLI | KIBUKUSU | KIKISA | KIISUKHA | KISWAHILI |
|---|---|---|---|---|
| /Kwivula/ | / xibula/ | / xwibula/ | /xwibula/ | Kuza |
| /lidiku/ | | | /litu x u/ | siku |
| /ilikudu/ | | /lixutu/ | /lixutu/ | Kobe |
| /umukɔ nɔ / | /kumuxɔnɔ/ | / ɔ muxɔnɔ/ | / muxɔnɔ/ | Mkono |
| /umukɑ: na | / muxɑnɑ/ | / muxana/ | /muxana/ | Msichana |
| /umukali/ | / muxasi/ | / muxasi/ | /muxali/ | Mwanamke |
| /amadak / | /kamataxɔ/ | /amataxɔ/ | /mataxɔ / | matakɔ |
| /uvudiku/ | | | /vutuxu/ | Usiku |
| /umukɔ:ɲɛ/ | | / mux :ɲɛ/ | /muxɔɲɛ/ | Miwa |
| /kwiguta/ | /xuxwikura/ | / xwikura/ | /xwikura/ | Kushiba |
| /s ɛka/ | /tsɛxa/ | / xutsɛxa/ | /xusɛxa/ | Kucheka |

Kuwepo kwa sauti /X/ katika lahaja za Kibukusu, Kikisa na Kiisukha na kukosekana kwa sauti hiyo katika lahaja ya Kilogooli kunachukuliwa na baadhi ya wasomi kama vile Angogo (1983) kama jambo lililohusisha mabadiliko ya kiisimu kwa wazungumzaji wa lahaja zinazohusika kihistoria. Kwao, sauti /k/ ambayo ni kipasuo ndiyo liyokuwepo hapo awali lakini ilianza kubadilika polepole na kuwa /x/ ambayo ni kikwamizwa. Hii ni sawa na sheria ya Grimm inayohusisha kutoghunisha kwa vipasuo ghuna na kubadilisha vipasuo visivyoghuna hadi kuwa vikwamizwa. Kwa hivyo:

[b]     [d]     [dz]     [g]

zitakuwa

[p]     [t]     [ts]     [k]

Sauti nyingine inayowasumbua Walogooli kutamka na ambayo hupatikana katika lahaja zile zingine tatu ni sauti ya kimandende /r/. Badala ya sauti hii, Walogooli hutumia sauti /t/ ambayo mara nyingi huwaacha wazungumzaji wa lahaja hizo zingine tatu kutojua maana ya maneno yanayotajwa mpaka waelezewe. Mifano ni kama ifuatayo:

| Kilogooli | Kibukusu | Kikisa | Kiisukha | Kiswahili |
|---|---|---|---|---|
| /lɛ : ta/ | /xurɛra/ | / xurɛra/ | /lɛra/ | leta |
| /jita/ | /jira/ | / xwira/ | /jira/ | ua |
| /uvutambi/ | | / burambi/ | /Burambi/ | urefu |
| /ikiguti/ | si: kuri | /ɛʃikuri / | /ʃikuri/ | uwanja |
| /imitugɔ/ | | | /mirukɔ/ | mifugo |
| /mutwi/ | /kumurwɛ/ | /ɔmurwɛ/ | /murwi/ | kichwa |
| /iligoti/ | | | /liŋɔri/ | shingo |
| /litu/ | /liru/ | / ɛʃirwi/ | /ʃirɔji/ | sikio |

Kutokana na mifano tuliyotaja hapo juu, maneno yafuatayo yaweza kukanganya kutokana na sababu hiyo. Neno /uvutambi/ la Kilogooli laweza kuchukuliwa na

Waisukha na vile vile Wabukusu kumaanisha ile hali ya kutokuwa na kitu badala ya maana inayokusudiwa ya "urefu".

Hali kadhalika, neno /mutwi/ la Kilogooli laweza kuwakanganya wabukusu na wakisa na kuwapa maana potovu badala ya ile inayokusudiwa ya 'kichwa' kwa sababu ya kukosekana kwa sauti hiyo ya /r / katika lahaja ya walogooli.

Licha ya hayo tunapata kuwa Walogooli wanapowasiliana na wabukusu, wao hupata shida kutamka sauti /ts/ ambayo haipatikani katika lahaja yao na hutumia sauti kikwamiza /z/ kama kibadala chake mifano ifuatayo itadhihirisha jambo hili.

| Kilogooli | Kibukusu | Tafsiri kwa kiswahili |
|---|---|---|
| /zia/ | /tsia/ | enda |
| /amazi/ | /kametʃi/ | maji |
| /umusaza/ | /musietʃa/ | mwanamume |
| /k :za/ | /xɔtʃa/ | mjomba |
| /ziŋganɒ/ | /tsiŋgano/ | hadithi |

Sauti nyingine ambayo huwatatiza Walogooli wanapowasiliana na Waisukha na Wakisa kuitamka ni kikwamizwa /g/. Sauti hii haipatikani katika lahaja hiyo kibadala chake huwa ni kizuiwa /k/. Kikwamiza /ʃ/ vile vile hakipatikani katika lahaja ya Wabukusu na kwa hivyo huwatatiza Wabukusu kuitamka na badala yake wao hutumiwa kikwamizwa /s/ kufidia ile /ʃ/.

Mifano ni kama ifuatayo:

| **Kilogooli** | **kibukusu** | **kikisa** | **kiisukha** | **kiswahili** |
|---|---|---|---|---|
| /kiguti/ | /sikuri/ | /ɛsikuri/ | /ʃikuri/ | uwanja |
| /ikibala/ | /sibala/ | | /ʃibala/ | dunia |
| /umukira/ | | / muʃira/ | /muʃira/ | Mkia |
| /ɛkɛdɛtɛ/ | | /ɛʃitɛrɛ/ | /ʃ itɛrɛ/ | kidole |
| /Ikiguru/ | /sikulu/ | /ɛʃikulu/ | /ʃikulu/ | mlima |
| /ikindu/ | /sindu/ | /ɛʃindu/ | /ʃindu/ | kitu |
| /ikihanwa/ | /sianwa/ | /ɛʃ ianwa/ | ʃihanwa/ | zawadi |

Hata hivyo waisukha na wakisa hawapati shida katika kutamka fonimu /k/na/ / kwani fonimu hizo zinapatikana katika jumla ya idadi ya sauti za lahaja hizo.

Hali kadhalika sauti nyingine isiyopatikana katika lahaja ya kilogooli ni kipasuo cha midomo kisichoghuna /p/. Sauti hii hutatiza walogooli sana wanapojaribu kuitamka. Kulingana na Guthrie (1967) badala ya kutamka sauti hii Walogooli huibadilisha na kikwamizwa cha midomo /b/. Tatizo la kuitamka sauti /P/ huwapata Walogooli wanapowasiliana na wenzao kutoka Isukha, Kisa, na Bukusu ambao wana sauti hiyo katika jumla ya idadi ya fonimu katika lahaja zao mifano.

| Kilogooli | Kibukusu | Kikisa | Kiisukha | Kiswahili |
|---|---|---|---|---|
| /kibaga/ | | /ɛlipaka/ | /lipaka/ | paka |
| /kuburuka/ | /puruxa/ | / xupuluxa/ | /xupuluka/ | puruka |
| /kuba/ | /xupa/ | /xupa/ | /xupa/ | piga |

Ni muhimu kusisitiza hapa kuwa, ingawa sauti /p/ hupatikana katika lahaja za kibukusu, kiisukha na kikisa ni maneno machache sana asilia katika lahaja hizi yanayotumia kipasuo /p/ mengi ni ya kiingereza au kiswahili na yaliyo toholewa kama inavyojitokeza katika mifano ifuatayo.

| Kiisukha | Kibukusu | Kikisa | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /ipasi/ | | | pasi |
| /xupambana/ | | | kupambana |
| /ipasia/ | | | pazia |

Kwa jinsi ambavyo Walogooli hutatizika sana katika kuitamka sauati kipasuo /P/ wanapowasiliana na wenzao, ndivyo ambavyo Waisukha, Wabukusu na Kikisa wanavyotatizwa kutamka sauti ya kipasuo /g/ hasa wanapowasiliana na Walogooli kwani sauti hiyo haipatikani katika lahaja hizo.

| Kiisukha | Kibukusu | Kikisa | Kilogooli | Kiswahili |
|---|---|---|---|---|
| /kumila/ | | | /gumila/ | shika |
| /jeka/ | /jaikala/ | / wijɛka/ | /jaga/ | kuna |
| /raka/ | | / xuraka/ | /ta:ga/ | panda |
| /kwa/ | /xukwa/ | / xukwa/ | /gwa/ | anguka |

| Kiisukha | Kibukusu | Kikisa | Kilogooli | Kiswahili |
|---|---|---|---|---|
| /kula/ | /kula/ | /ɔxukula/ | /gura/ | nunua |
| /ikasi/ | | | /igasi/ | kazi |
| /likɔndi/ | | /likɔndi/ | /iligɔndi/ | kondoo |

Vile vile Waisukha, Wakisa na Wabukusu hupata shida kutamka sauti /d/ wakati wanapowasiliana na Walogooli, kwani sauti hiyo haipatikani katika lahaja zao. Kila mara wanapojaribu kuitamka sauti /d/, wao huishia kuitamka kama /t/ kwa mfano.

| Kilogooli | Kiisukha | Kikisa | Kibukusu | Kiswahili |
|---|---|---|---|---|
| /mɛ: da/ | /mɛ:ta/ | / xumɛta/ | | Ongeza |
| /ilidiku/ | /lituxu/ | | | Siku |
| /ilikudu/ | /lixutu/ | /lixutu/ | /liʧutu/ | Kobe |
| /ɛkɛdɛtɛ/ | /ʃitɛrɛ/ | /ɛʃitɛrɛ/ | | Kidole |
| /uvudiku/ | / utuxu/ | | | Usiku |
| /uvudɔhi/ | /ɬutɔji/ | /amatɔji/ | /kamatɔʃi/ | Udongo |
| /bidididi/ | /ʃititi/ | /ʃititi/ | | vichache |

Kwa hivyo utapata kuwa, ikiwa Waisukha, wangependa kulitamka neno /uvudiku/ jinsi Walogooli wanavyolitamka, wataishia kulitamka kama /uvutuhu/ kwa vile hawana sauti /d/ na vile vile wao hupendelea sauti /x/ kuliko sauti /k/ kama tulivyoeleza hapo mbeleni.

Kwa upande mwingine kuna sauti /ʝ/ ya lahaja ya kibukusu ambayo kwayo matumizi yake katika lahaja hiyo huwafanya wale wanozungumza lahaja hizo zingine za Isukha, Kisa na Logooli wasiweze kufahamu kabisa maana ya neno ambamo sauti hiyo imetumika.

| Kibukusu | Kilogooli | Kikisa | Kiisukha | Kiswahili |
|---|---|---|---|---|
| /jaʃʝa/ | /ta:ŋga/ | /ɔxuʃaka/ | /raŋga/ | Anza |
| /ɛʝaʝa/ | /lʝa:nza/ | | / lʝanza/ | Ziwa |
| /□ u/ | /inzu/ | /inzu/ | /inzu/ | Nyumba |

Mfuatano wa sauti /e/ na /ʝ/ hufanya maana ya neno linalotamkwa lipotoke, neno hilo linaposikilizwa na wazungumzaji wa lahaja hizo zingine kwani ni mfuatano wa sauti ulio nadra sana kwa wazungumzaji wa lahaja hizo zingine tatu. Kwa mfano neno / ɛʝaʝa/ linaweza kuchukuliwa na Waisukha au Wakisa au Walogooli kuwa ni /janza/ ambayo ina maana tofauti ya" kufurahi".

Kuna pia sauti kikwamizwa /f/ ambayo hutimika kwa wingi na wazungumzaji wa lahaja za kikisa na kibukusu. Ingawa sauti hii sio ngumu kutamkwa na wazungumzaji wa kiisukha wala kilogooli, shida ni kwamba mahali ambapo sauti /f/ hutumika katika Kikisa na Kibukusu, Waisukha na Walogooli hutumia kikwamizwa /ɸ/ ambayo ni sauti inayokaribiana na /f/ kimatamshi. Vileveile wao hutumia vibadala vingine kama vile /mb/, /k/, /r/. kwa mfano

| Kikisa | Kibukusu | Kiisukha | Kilogooli | Kiswahili |
|---|---|---|---|---|
| / xufwa/ | /lifwa/ | /lixutsa/ | /ilikuza/ | Kifo |
| /ifula/ | /ɛfula/ | /imbula/ | /imbula/ | mvua |
| / luβafu/ | /luβafu/ | /luβalu/ | /zimbalu/ | Mbavu |
| /ɣlufu/ | /lufumbi/ | /lukuʃi/ | /uluguki/ | vumbi |

Tukitazama mifano tuliyotoa hapo juu tunapata kuwa sauti (fonimu) /f/ ni konsonanti inayojitokeza katikati ya irabu mbili au katikati ya irabu na nusu irabu za mzizi wa jina ikitumika katika maneno ya kibukusu na kikisa. Katika maneno ya kiisukha na Kilogooli sauti/f/ haiwezi kujitokeza katika nafasi hiyo na kwa hivyo wazungumzaji wa lahaja hizo mbili hawewezi kuitamka sauti /f/ kimakosa wala kimaksudi ikiwa itajitokeza katika nafasi kama hiyo.Hili ni jambo ambalo halimo akilini mwao.. Kwao, sauti /f/ hujitokeza tu mwanzoni mwa mzizi wa jina kama inavyodhirisha na mifano ifuatayo

| Kiisukha | Kilogooli | Kiswahili |
|---|---|---|
| /fwana/ | /fwana/ | Fanana |
| /fuŋga/ | /fuŋga/ | Funga |
| /fwala/ | /fwala/ | Vaa |

Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa matumizi tofauti ya sauti /f/ katika lahaja za Kibukusu na Kisa ikilinganishwa na zile za Kilogooli na Kiisukha ni swala linalohusisha tofauti za kimuundo katika fonolojia za lahaja hizo. Baadhi ya wasomi (Laver 1967), Trudgill & Laver (1979), Abercrombie (1967) wamesisitiza kwamba wazungumzaji wa lugha au lahaja fulani hupata ugumu mkubwa sana kutamka sauti fulani ikiwa zina mfuatano ambao hawajauzoea katika mazungumzo yao ya kila siku.

Kwa muhtasari hizo ndizo shida za kimatamshi zinazowakumba wazungumzaji wa lahaja hizi wanapowasiliana.

# SURA YA TANO

# TOFAUTI ZA KIMOFOLOJIA: UTATA UNAOSABABISHWA NA VIAMBISHI VYA VITENZI

## 5.1 Utangulizi

aina ya maneno ambayo hutumika kama sehemu muhimu sana ya kiarifa cha Vitenzi ni sentensi na ambavyo huarifu/hueleza jambo fulani linalohusu kiima cha sentensi. Kulingana na Richards etal (1985), kitenzi ni neno ambalo hutokea kama sehemu muhimu ya kiarifa na ambalo huambishwa mofu za njeo, hali, nafsi, idadi, kauli na dhamira. Aidha vitenzi hueleza juu ya tendo au hali.

Kama lugha nyingi za kibantu, vitenzi vya lahaja mbalimbali za wabaluyia huambishwa viambishi awali na viambishi tamati. Hata hivyo tunapozingatia jamii hiyo tunapata kwamba watu wanaoongea lahaja tofauti, hutumia mofu tofauti kuambisha vitenzi ili kuonyesha hali, nafsi, idadi, njeo, kauli na dhamira. Vile vile mofu zinazoambishwa vitenzi, mara nyingine huweza kubeba maana moja katika lahaja moja na wakati huo huo, kubeba maana tofauti kabisa katika lahaja nyingine. Mambo haya huzua shida wakati watu wa lahaja hizi wanapowasiliana kwani wazungumzaji wa lahaja tofauti hukumbana na mofu mpya wanapowasiliana ambazo huambishwa vitenzi na ambazo hawajazizoea katika matumizi yao ya kila siku. Mifano ifuatayo kutoka lahaja za Kilogooli, Kibukusu, Kikisa and Kiisukha itadhihirisha jambo hili.

## 5.2 VIAMBISHI VYA UYAKINIFU

### NAFSI YA KWANZA

| Kiswahili | Kikisa | Kilogooli | Kiisukha | Kibukusu |
|---|---|---|---|---|
| Nilipika | Ndatekha | Ndadeka | Natekha | Natekha |
| Tulipika | Khwatekha | Kwadeka | Khwatekha | Khwatekha |
| Ninapika | Endekhanga | Ndeka | Ndekhanga | Khendekha |
| Tunapika | Khutekhanga | Kudeka | Khutekhanga | Khulikho- Khutekha |
| Hupika(umoja) | Amalanga Atekha | Madeka | Amatekha | Atekhanga |
| Nimepika | Endeshere | Ndakadeka | Ndeshi | Natekhile |
| Tumepika | Khuteshere | Kwadodeka | Khuteshi | Kwatekhile |
| Hupika(wingi) | Khumalanga Khutekha | Makodeka | Khumakhutekha | Khutekhanga |
| Anapika | Atekhanga | | Atekhanga | |

Kwa kutazama jedwali hii vizuri, tunapata kuwa kitenzi halisi ni 'pika' ambacho kisawe chake ni 'tekha' katika Kikisa, Kiisukha na Kibukusu. Kisawe cha 'pika' katika kilogooli ni 'deka'. Mizizi na viishio ya maneno haya ni kama ifuatayo:

Kiswahili - {Pik} + {a}

Kilogooli - {dek} + {a}

Kiisukha, Kibukusu, Kikisa - {tekh} + {a}

Maumbo yale mengine tutayachakulia kuwa viambishi awali au viambishi tamati vinavyoambishwa kwa mizizi ya maneno.

Katika lahaja ya Kiisukha na Kikisa, neno lenye kisawe 'anapika' ni 'Atekhanga' viambishi vinavyounda neno hili ni kama vifuatavyo:

{A} - Kiambishi awali cha kuonyesha nafsi (yeye mmoja)

{tekh} - Mzizi wa kitenzi

{ang} - Kiambishi tamati cha kuonyesha hali ya kuendelea

{a} - Kiishio

Vilevile, katika lahaja hizo za Kiisukha na Kikisa neno lenye kisawe 'Tunapika' ni 'khutekhanga'. Viambishi vinavyounda neno hili ni vifuatavyo:

{khu} - Kiambishi awali kinachoadhiria nafsi na idadi (sisi – wengi)

{tekh} - Mzizi wa kitenzi

{ang} - Kiambishi tamati cha kuonyesha hali ya kuendelea

{a} - kiishio

Kwa upande mwingine maneno hayo mawili hutumika vilevile katika lahaja ya Kibukusu na viambishi vinavyounda maneno hayo in kama vifuatavyo.

'Atekhanga'

{A} - Kiambishi awali cha kuonyesha nafsi na idadi (yeye – mmoja)

{tekh} - Mzizi wa kitenzi

{ang} - Kiambishi tamati cha kuonyesha hali ya kurudiwarudiwa

{a} - Kiishio

'Khutekhanga'

{Khu} - Kiambishi awali cha kuonyesha nafsi na idadi ( Sisi wengi)

{tekh} - Mzizi wa kitenzi

{ang} - Kiambishi tamati cha kuonyesha hali ya kurudiwarudiwa

{a} - Kiisho

Tukilinganisha vitenzi hivyo kwa kuzingatia Waisukha na Wakisa kwa upande mmoja na wabukusu kwa upande mwingine tunapata kuwa kiambishi tamati {ang} ni kiambishi kinacholeta utata kwa pande zote mbili. Hii ni kwa sababu kiambishi hicho kinabeba maana mbili tofauti tunapozingatia lahaja hizo.

Katika lahaja za Kiisukha na Kikisa, mtu asemapo neno 'Atekhanga' anamaanisha kuwa kuna mtu ambaye anaendelea na kitendo cha 'Kutekha' (Kupika). Vile vile anaposema 'Khutekhanga' (tunaendelea kupika).

Kwa upande mwingine, maneno haya yataeleweka kivingine kwa Wabukusu, kwani kwao 'Atekhanga' inamaanisha kuwa 'yeye hupika kila wakati na 'khutekhanga' inamaanisha 'Sisi hupika kila wakati.

Kwa hivyo maneno haya yakitumika wakati watu hawa wanapowasiliana, hubeba maàna tofauti kwa makundi haya mawili ya wazungumzaji. Kwa ujumla twaweza kusema kuwa vitenzi vyote vya hali ya uyakinifu vilivyo na kiambishi tamati {ang} huleta utata tulioeleza hapo juu kwa makundi hayo mawili ya wazungumzaji

### 5.3 VIAMBISHI VYA UKANUSHI

<u>**NAFSI YA KWANZA**</u>

| **Kiswahili** | **Kikisa** | **Kilogooli** | **Kiisukha** | **Kibukusu** |
|---|---|---|---|---|
| Sikupika | Shindateshere tawe | Ndeki mba | Ndeshi tawe | Senatekha tawe |
| Hatukupika | Shikhwateshere tawe | Kudechi mba | Khuteshi tawe | Sendetekha tawe |
| Sipiki | Shendekha tawe | Ndeka Mbaa | Ndekha tawe | Sendetekha |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | tawe |
| Hatupiki | Shikhuutekha tawe | Kudeka mba | Khutekha tawe | Sekhutekhanga tawe |
| Sijapika | Eshiri okhutekha | Nkiri kudeka | Shiri khutekha | Sekhwatekhile tawe |
| Hatujapika | Khushiri okhutekha | Kukiri kudeka | Khushiri kutekha | Sekhwatikhule tawe |

Katika kukanusha vitenzi vya lahaja hizi maneno mengine pamoja na viambishi huambatanishwa na kitenzi ili kuleta dhana ya ukanushi. Kama tulivyoonyeshwa katika jedwali yetu hapo juu.

Kwa muhtasari, wazungumzaji wa lahaja ya kibukusu wanadai kuwa hawawezi kuelewa kama Walogooli wanokanusha kitend fulani lakini uchunguzi wetu unaonyesha kuwa shida kuu inatokana na wazo la kukosekana kwa baadhi ya sauti katika lahaja za Kibukusu na ambazo ziko katika lahaja ya Kilogooli kwa mfano sauti /d/ na /k/. Kwa hivyo Mlogooli akisema /ndeki /, inakuwa in vigumu kwa Mbukusu kufasiri neno hili.

Wakati huohuo, wazungumzaji wa lahaja za Kikisa, Kiloogoli na Kiisukha hupata shida nyingi wanapojaribu kufasiri ukanushi wa maneno ya Kibukusu. Jambo hili limetokana na matumizi yao ya kiambishi awali {Se} ambacho hakipatikani katika lahaja hizo zingine.

Hata hivyo shida kuu hutokea baina ya Wakisa na Wabukusu wakati ukanushi katika nafsi ya kwanza katika kikisa unafanywa kwa kuambatanisha kike kitenzi na neno "eshiri" kwa mfano ' eshiri okhutekha' yaani (bado) sijapika. Ukanushi huu upo katika hali timilifu. Viambishi vinavyounda neno hilo ni {e}+ {shiri}

{e} - Mimi

{Shiri} - bado

Na katika lahaja ya Kibukusu viambishi vinavyounda neno hilo ni {e}+ {sili} kwa vile sauti /ʃ/ itatamkwa kama /s/ na vitaashiria maana zifuatazo

{e} - Kitu

{sili – bado

Kutokana na maelezo hayo tunapata kuwa Wakisa wanaposema "eshiri Okhutekha" kumaanisha" mimi bado sijapika" Wabukusu wanafasiri maneno hayo kumaanisha kifaa hakijapika. Matumizi ya kiambishi {e} yanakanganya sio tu katika vitenzi vya ukanushi bali pia katika vitenzi vya uyakinishi. Mfano

Kikisa – Ehandikanga – Ninaandika

Kibukusu – Ehandikanga – Kifaa kinachoandika kila mara (Kumbuka matumizi ya Kiambishi tamati {ang}

| Kiswahili | Kikisa | Kiisukha | Kilogooli | Kibukusu | |
|---|---|---|---|---|---|
| Nilikuwa Ninaenda | Ndali Nehandikanga | Nali nimbandikanga | Ndali nimbandika | Nabele ndikho mbandika | |
| Lilokuwa Linarushwa | Liali nilisukunungwa | Liali lileswanga | Liali Lilaswa | Liabele khalimatwa | |
| Yalikuwa yakimwagwa | Kali kasundulwangwa | Gari kasundulwa | Kali Kasundulwanga | Kabele khakachukhwa | |
| Kilikuwa Kikiibiwa | Shiali shibungwa | Shali Shihubwangwa | Kali kihubwa | Shabele Khasibwa | |

Katika hali ya kuendelea, njeo iliyopita, kiambishi {li} katika neno linalotangulia kitenzi ndicho kinachotumika kuonyesha njeo iliyopita katika lahaja za Kikisa na Kiisukha nayo Kilogooli ina kiambishi {- li} ambacho ni kibadala cha {-li}. Kwa upande mwingine Kibukusu kina { - bele} kuashiria njeo hiyo. Hata hivyo matumizi ya { - bele} kwa Wabukusu huwakanganya wazungumzaji wa lahaja hizo zingine tatu kwani kwao { - bele} huashiria hali timilifu na wala sio njeo iliyopita. Kwa hivyo wakati Kibukusu kinatumia { - bele} kuashiria wakati uliopita, wazungumzaji wa lahaja hizo zingine watachukuwa kuwa njeo inayozingatiwa ni wakati uliopita sio muda mrefu na kwa hivyo hawataelewana kuhusiana na swala la njoo. Hata hivyo viambishi vingine vya hali havina utata unaosababisha kutoelewana miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja hizi wanapowasiliana.

## 5.5 VIAMBISHI VYA VITENZI VYA KAULI

Nyingi ya viambishi vya vitenzi vya kauli vya lahaja hizi nne hufuata mfumo sawa kama ule wa lugha ya Kiswahili na kwa hivyo hazina matatizo mengi wakati wazungumzaji wanapowasiliana kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

**Viambishi vya vitenzi vya kunyambua**

**Kauli ya kutenda**

| **Kiswahili** | **Kikisa** | **Kilogooli** | **Kiisukha** | **Kibukusu** |
|---|---|---|---|---|
| Soma | Soma | Soma | Soma | Khulikho-<br>Khusoma |
| Cheza | Buya | Kina | Baya | Ndikho-niya |
| Ruka | Ruma | Sira | Ruma | Alikho auna |
| Chora | Chora | Chora | Chora | Mulikho-chora |

**Hali ya kutendwa**

| **Kiswahili** | **Kikisa** | **Kilogooli** | **Kiisukha** | **Kibukusu** |
|---|---|---|---|---|
| Pigwa | Khupwa | Kubwa | Khupwa | Khuywa |
| Imbwa | Imbwa | Yimbwa | Yimbwa | Yimbwa |
| Chezwa | Baywa | Kinwa | Baywa | Inyawa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Somwa | Somwa | Somwa | Somwa | Somwa |
| Pelekwa | Yirwa | Shirwa | Yirwa | Tilwa |

Kauli ya kutendeka

| **Kiswahili** | **Kikisa** | **Kilogooli** | **Kiisukha** | **Kibukusu** |
|---|---|---|---|---|
| Pikika | Okhutekhekha | Dekeka | Khutekhekha | Tekhekha |
| Someka | Somekha | Someka | Somekha | Somekha |
| Chezeka | Bayike | Kukinika | Bayikha | Yinyakha |
| Imbika | Imbikha | Yimbika | Imbikha | Yimbikha |
| Choreka | Chorekha | Choreka | Chorekha | Chorekha |

**Kauli ya kutendesha**

| **Kiswahili** | **Kikisa** | **Kilogooli** | **Kiisukha** | **Kibukusu** |
|---|---|---|---|---|
| Chekesha | Tseshesia | Sekiza | Seshitsa | Chekhusia |
| Kopesha | Kopia | Gobiza | Kopitsa | Yekoposia |
| Tanyisha | Kholwa | Koriza | Kholitsa | Khosia |
| Chezesha | Bayiyia | Kiiniza | Bayitsa | Vinyanyia |
| Lisha | Lisia | Rihiza | Lishitsa | Lisie |
| Somesha | somia | Sominya | Sominya | Somia |
| Rukisha | Rumia | Tuminya | Ruminya | Sunia |

Hata hivyo, tunapotazama kauli ya kutendesha tunapata shida Fulani. Kauli hii, kulingana na Mgullu (1999) hutumiwa hasa wakati ambapo uko uhusika wa aina mbili yaani moja kuna mtu/watu wanaowafanya watu/mtu mwingine afanye jambo fulani. Huyu si lazima atende jambo analowafanya watu wengine walifanye. Pili ni kuwa kuna mtu au watu wanaofanywa wafanye tendo fulani na mtu mwingine. Hawa ni lazima walitende jambo hilo.

Kwa hivyo tunapotazama orodho yetu ya vitenzi katika kauli ya kutendesha tunapata kuwa viambishi tamati vifuatavyo hutumika katika kila lahaja kuwasilisha kauli hiyo na kwa hivyo uhusika tulioutaja hapo juu.

| <u>LAHAJA</u> | <u>VIAMBISHI</u> |
|---|---|
| Kikisa | {i} |
| Kilogooli | {iz} na {iny} |
| Kiisukha | {its} na {iny} |
| Kibukusu | {i} |

Wazungumzaji wa lahaja za Kiisukha na Kilogooli walidai kuwa mara nyingi ni vigumu kwao kujua kuna kauli inayozingatiwa ni ya kutendesha wakati ambapo Wabukusu na

Wakisa wanatumia kiambishi tamati {i}peke yake kueleza kauli hiyo, kwani wao wamezoea kutumia viambishi tamati tulivyotaja hapo juu ili kueleza kauli hiyo ya kutendesha.

## 5.6 UTATA UNAOSABABISHWA NA KISABIKI KIAMBISHI AWALI (PRE-PREFIX){KU}KATIKA NOMINO ZA KIBUKUSU

Licha ya mizizi, baadhi ya nomino za lahaja tunazozingatia yaani Kiisukha, Kilogooli, Kikisa na Kibukusu huwa na viambishi awali ambavyo huwekwa kabla ya mizizi, kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

| Kiswahili | Kibukusu | Kikisa | Kilogooli | Kiisukha |
|---|---|---|---|---|
| Mkono | {Ku}mukhono | {O}mukono | {U}mukono | Mukhono |
| Kichwa | {Ku} murwe | {O}murwe | {U}mutwi | Murwi |
| Kisu | {Ku} bano | {O}mbano | {U}mbano | Mmbanu |
| Mdomo | {Ku}munwa | {O}munwa | {U}munwa | Munwa |
| Mkia | {Ku}mukhinga | {O}mushira | {U}mukila | Mshila |

Kwa hivyo tunaona kuwa katika baadhi ya nomino Kibukusu kina kisabiki kiambishi awali {Ku}, Kikisa kina kiambishi awali {O}, Kilogooli kina kiambishi awali {U} na

Kiisukha mara nyingi hakina kiambishi awali kwenye nomino. Hata hivyo tunapata kuwa matumizi ya kiambishi awali {Ku}katika baadhi ya nomino za Kibukusu huwafanya wazungumzaji wa lahaja zilizosalia tatu kufikiria kuwa nomino inayotajwa inazingatiwa katika hali yake ya ukubwa kwani matumizi ya kiambishi awali {Ku} katika nomino za lahaja hizo huashiria dhara ya ukubwa. Kwa mfano:

| Kiswahili | Kikisa | Kilogooli | Kiisukha |
|---|---|---|---|
| Kisu Kikubwa | Kubano | Gubano | Kubanu |
| Kichwa Kikubwa | Kurwe | Gutwi | Kurwi |
| Mdomo Mkubwa | Kunwa | Gunwa | Kunwa |

Kwa hivyo wakati Wabukusu wanapotaja nomino katika hali yake ya kawaida, wazungumzaji wa lahaja hizo zingine hufasiri nomino hiyo kuwa katika hali yake ya ukubwa jambo ambalo ni potovu.

## 5.7 TOFAUTI ZA NGELI

Wataalamu mbalimbali wa sarufi wana njia tofauti za kupanga nomino katika ngeli mbalimbali .Hata hivyo, lahaja za kiluyia zinapogawanywa katika ngeli kwa kutumia kigezo cha kimofolojia ya nomino ,kinachozingatiwa zaidi ni viambishi awali vya idadi vya umoja na wingi vinavyotimiwa. Katika uanishi huu ni vile viambishi vya umbo la

kawaida la nomino na siyo viambishi awali vya idadi ya umoja na wingi katika nomino hizo.Aidha viambishi awali vya umoja na wingi vinavyotumiwa katika uanishaji huu ni vile viambishi vya umbo la kundi la nomino na sio viambishi awalivya ukubwa au udogo wa nomino hizo vinavyozingatiwa.Kulingana na Mgullu (1999)kwa kuzingatia kigezo cha viambishi awali katika nomino, ngeli nomino ya kimofolojia (morphological noun class) itakuewa na maana ya :

Kundi moja la nomino zilizo na viambishi vya umoja na /au vya wingi vinavyo fanana .

Huku tukirejelea lahaja nne tunazozishghulikia yaani; Kiisuka,Kibukusu,Kikisa na Kilogooli na kwa kuzingatia yale tulioeleza hapo juu,ngeli zifuatazo za kimofolojia zinaibuka .

a)Ngeli ya Mu-Ba

Katika ngeli hii, maneno katika hali ya umoja huanza na kiambishi awali mu na katika hali ya wingi huanza na kiambishi awali Ba.Hata hivyo katika baadhi ya lahaja nomino huwa zina kisabika kiambishi awali u\o katika umoja na a\ ba katika wingi

Mifano.

| Kiwahili | Kiisukha | Kilogooli | Kibukusu | Kikisa |
|---|---|---|---|---|
| Mtu | Mundu | Umundu | Umundu | Omundu |
| Watu | Bandu | Avandu | Abandu | Abandu |
| Mzee | Musakuhulu | Umusakulu | Omusakulu | Omukofu |
| Wazee | Basakhulu | Avasakulu | Basakhulu | Abakofu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mtoto | Mwana | Umwana | Omwana | Omwana |
| Watoto | Baana | Avaana | Baana | Abana |

Kundi hili la nomino hueleweka vyema kwa wazungumzaji wa wa lahaja zote nne.

b)Ngeli ya Mu-Mi.

Nomino katika kundi hili huanza na kiambishi awali Mu katika hali ya umoja na kiambishiawali Mi katika hali ya wingi.Hata hivyo baadhi ya nomino zina kisabiki kiambishi awali Ku\u katika hali ya umoja na Ki\i katika hali ya wingi.

Mifano:

| Kiswahili | Kiisuka | Kilogooli | Kibukusu | Kikisa |
|---|---|---|---|---|
| Mti | Musala | Umusala | kumurongoro | Omusala |
| Miti | Misala | Imisala | Kimirongoro | Imisala |
| Mlango | Muliango | Umuliango | Kumuliango | Omuliango |
| Milango | Miliango | Imiliango | Kimiliango | Emiliango |
| Msitu | Muliru | Umuritu | Kumusuru | Omusiro |
| Misitu | Miliru | Imiritu | Kimisuru | Misiro |

Kwa ujumla, isipokuwa kwa sababu ya tofauti za kimsamiati na tofauti za kisabiki kiambishi awali {ku} na {ki} katika lahaja ya kibukusu ambazo hukanganisha tunapozingatia dhana ya ukubwa na udogo, (swala ambalo tumekwisha lizingatia hapo awali), kundi hili la nomino hueleweka waziwazi kwa wazungumuzaji wa lahaja hizi nne.

Ngeli ya i/e –chi/tsi

| Kiswahili | Kiisuka | kilogooli | Kibukusu | Kikisa |
|---|---|---|---|---|
| Jicho | Imoni | Emoni | Emoni | Imoni |
| Macho | Tsimoni | Itsimoni | Chimoni | Simoni |
| Ng'ombe | Ing'ombe | Eng'ombe | Ekhafu | Ing'ombe |
| Ng'ombe (wingi) | Tsing'ombe | Itsing'ombe | Chikhafu | Tsing'ombe |
| Nyumba(umoja) | Intsu | Inyumba | Enju | Inzu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Nyumba(wingi) | Tsintsu | Itsinyumba | Chinju | Tsinzu |

Wazungumzaji wa lahaja hizi nne huweza kuelewa bila matatizo mengi, iwapo maneno katika kundi hili yanatumika katika hali ya umoja au wingi.

Ngeli ya ki\shi-Bi

Mifano ya nomino katika ngeli hii ni kama ifuatayo

| Kiswahili | Kiisukha | Kilogooli | Kibukusu | Kikisa |
|---|---|---|---|---|
| Kiti | Shisako | Ikisala | Shisala | Shisala |
| Viti | Bisako | Ibisala | Bisala | Bisala |
| Kikapu | Shikapu | Ikikabo | Sikapu | Shikapu |
| Vikapu | Bikapu | Ivikabo | Bikapu | Bikapu |
| Kitabu | Shitapu | Ikitapu | Sitapu | Shitabu |
| Vitabu | Bitapu | Ivitabu | Bitapu | Bitapu |

Kundi hili la nomino kama makundi yale mengine halikanganyi wakati wa kuzingatia nomino katika hali ya umoja na vile vile katika hali ya wingi.

Tukichukua makundi haya ya manne ya nomino kama kiwakilishi cha makundi mengine ya nomino katika lahaja hizi nne,tunaweza kufikia uamuzi kuwa ngeli za kimofolojia katika lahaja hizi nne hazizui matatizo mengi, watu wa lahaja hizi wanapowasiliana.

Vilevile,tungependa kusisitiza kuwa ugawanyaji wa nomino katika makundi tofauti katika lahaja hizi nne yaani Kiisukha,Kikisa,Kibukusu na Kilogooli hutegemea zaidi kigezo cha kimofolojia.Ukubaliano wa kisarufi hauzingatiwi kama inavyo dhihirika katika sentensi zifuatazo.Kiambishi awali cha nomino ndicho huamua viambishi vitakavyotumika katika maneno yatakayofuata ya Kiisukha;

1)Tsing'ombe yitsi tsilakhutsa

Ng'ombe hawa watakufa

2)Tsinzu yitsi tsilakwa .

Nyumba hizi zitaanguka .

Katika sentensi ya kwanza tunazingatia ng'ombe ambao ni viumbe walio na uhai .Katika sentensi ya pili tunazingatia nyumba ambacho ni kitu kisicho na uhai ,lakini tunapoandika sentensi, ukubaliano wa kisarufi ni sawa .Hakuna tofauti katika vimbishi awali.

Jambo hili ni kinyume na maoni ya wasomi kama vile Mgullu(1999),Waihiga(1999) na Mbaabu(1992)wanaopendekeza utumiaji wa kigezo cha kisintaksia katika uainishaji wa ngeli.

# SURA YA SITA

## TOFAUTI ZA KISIMU-JAMII

### 6.1 Kuhusu utafiti

Njia ambayo ilitumika kikamilifu kwa utafiti huu ni ya hojaji .Ni muhimu kutangulia kutaja kuwa hojaji ni za aina mbili .kuna hojaji ambayo kwayo mhojaji anatakiwa kuyajibu maswali kwa njia ya kuandika. Pili kuna hojaji ambayo mhojiwa anaulizwa maswali huku mhojaji akiandika majibu mwenyewe .

Tungependa kumjulisha msomaji kuwa katika kazi hii,aina zote mbili zilitumika. Katika sampuli yetu kuna wahojiwa ambao kiwango chao cha elimu kiliku cha chini sana .Kwa sababu hiyo ,utafiti haungefanywa kwa njia nyingine bali tu kwa kuwasomea wahojiwa maswali na kuyaandika majibu yao jinsi walivyosema. Hata hivyo wahojiwa wa aina hii walikuwa wachache mno .Kwa hivyo hojaji aina ya kwanza ambapo wahojiwa walipewa hojaji na kujibu maswali hayo wenyewe bila usaidizi wa moja kwa moja na mtafiti ndiyo iliyotumika zaidi .

Kwa vile idadi ya watu waliohusishwa na utafiti hii ni kubwa mno, hatungeweza kuwashughulikia wote na kwa hivyo tiliamua kuchagua sampuli kutoka miongoni mwao kwa kutumia mbinu ya bahati nasibu. Kwa kutumia mbinu hiyo tuliweza kupata wawakilishi wa wazungumzaji kutoka kila lahaja .Kutoka kila lahaja sampuli ya watu ishirini ilichaguliwa kama ifuatayo.

1)wazee ( umri zaidi ya miaka 45)

wanaume-4

wanawake-4

2)vijana

wavulana-4

wasichana-4

3)Elimu

wasio na elimu yoyote ya shule –2

Elimu ya sekondari na zaidi –2

Kabla ya kuingilia uchanganuzi wa matokeo ya utafiti huu tungependa kutaja matatizo matatu ambayo yalimkabili mtafiti wakati wa kuishughulukia kazi hii.

1)Si wahojiwa wote waliokuwa tayari kusaidia kujibu maswali haya. Wengine hawakuona haja ya kuyajibu maswali mpaka wajue nia na dhamira ya kazi yenyewe kwa hivyo ilimbidi mtafiti kuwashawishi kwa moyo wenye subira nyingi sana .

2)Kwa kukosa kuona umuhimu wa kuyajibu maswali, baadhi ya wahojiwa waliisha kutoa majibu chapwa ,ambayo kwa maoni ya mtafiti hayakusaidia sana utafiti huu.

3) Tulipodhamiria kufanya utafiti huu tulijua wazi kuwa hojaji au mawasiliano yetu yangekuwa katika lugha ya kiswahili hata hivyo idadi ya wahojiwa (Asili mia hamsini na tano )waliungama kuwa hawakuielewa lugha hiyo vyema,na kwa hivyo kutufanya kutfsiri hojaji hadi lugha hizo za kiswahili na kiingereza. Ilitubidi kutafuta wakalimani ili waweze kuwahoji katika lahaja zao mbalimbali.Matatizo haya yaliturudisha hatua nyingi nyuma.

Tungependa kusisitiza kuwa imetulazimu kuyataja mambo haya ili msomi au wasomi wa sehemu hii ya utafiti wetu kuweza kuelewa kuwa maamuzi tuliyoyafikia katika sehemu yalifikiwa baada ya kuzingatia mambo yote tuliyoyataja hapo juu . hojaji

## 6.2 TAASUBI /MITAZAMO TOFAUTI INAYOSHKILIWA NA WAZUNGUMZAJI WA KILA LAHAJA

Swala la taasubi /mitazamo ya lugha inayoshikiliwa na wazungumzaji wa lugha au ánuwai za lugha ni muhimu haswa tunapozingatia simu jamii. Kuna ushahidi kuwa mitazamo /taasubi za lugha zinazoweza zikaathiri jinsi walimu wa lugha wanavyoshughulikia wanafunzi wao (Lambert 1973; Seligman ,Turker na Lambet 1973) Vilevile ushahidi mwingne wapendekeza kuwa taasubi za lugha zaweza zikaathiri.Kujifunza kwa lugha (au anuwai ya lugha )ya pili (kwa mfano Lambert et al 1968). Kuongezea kwa hayo ushahidi mwingine umeonyesha ya kuwa taasubi za lugha zaweza kuwa na athari kwa anuwai mbili au zaidi kwa kuonyesha ikiwa wazungumzaji wa anuwai hizo wanaelewana au la (kwa mfano Wolff 1957)taasubi hizi za lugha zinahusisha mitazamo inayoelekezewa wazungumzaji wa lugha au anuwai zaidi na sio lugha peke yake .

Kulingana na Saville-Troike (1989), njia mojawapo ambapo taasubi hizi hujitokeza ni kupitia shutuma au madai ambayo hutolewa na

wazungumzaji wa lugha (au anuwai ya lugha )moja dhidi ya wenzao (stereotypes). Hebu tugeukie lahaja tunazozishughulikia, yaani Kibukusu, Kilogooli, Kikisa na Kisukha ili kuweza kuelea maadai haya.

Tukianza na Walogooli,tunapata kuwa wengi waliohojiwa isipokuwa walogooli wenyewe walidai kuwa wazungumzaji wa lahaja hiyo ni wazembe . Pia walidai kuwa ni kundi la watu waliopendelewa kujitenga kutoka kwa wazugumzaji wengine wa taifa la Wabaluyia .Vilevile walogooli wanachukuliwa kama watu wasioweza kutegemewa ka jambo lolote lile .Mwisho ,wengi wa wanaozungumza lahaja ya Kibukusu walidai kuwa namna ya kuzüngumza kwa Walogooli ilikuwa ya kitoto.Ni kutokana na wazo hili ambapowengi wa Wabukusu walieleza kuwa hawakuwana haja ya kujifunza lahaja ya Kilogooli kwa vile walichukuwa kuwa ni ya kitoto .Kiuchumi , Wabukusu walijona kama matajiri waliomiliki mashamba makubwa makubwa kinyume na wenzao Walogooli ambao walichukulia kuwa maskini kutokana na wazo kuwa walikuwa na idadi kubwa ya watu walioishi katika vijishamba vidogovidogo na hata huamia maeneo walikoishi wabukusu kama vile Kitale kuongezea kwa hayo Wabukusu walijiona kama matajiri waliojishughulisha na kilimo cha mahindi katika mashamba makubwa makubwa , jambo lililo wapa uwezo mkubwa kiuchumi , ikilinganishwa na Walogooli .

Kutokana na madai haya ,Wabukusu, wanajichukulia kama watu walio katika daraja la juu hasa kijamii na kiuchumi jambo ambalo huwafanya kutoshirikiana na wazungumzaji

wa lahaja zingine na haswa Walogooli kwa kiwango kikubwa kwa sababu tulizozitaja hapo juu.

Kwa ujumla twaweza kusema kuwa Walogooli na Wabukusu hudai kuwa hawaelewani kabisa wanapowasiliana kwa sababu ambazo tumetaja hapa juu ambazo zinatokana na taasubu wanazoshikilia na wala sio za kiisimu kwa vile utafiti wetu wa hapo awali wa kiulinganisha ulidhibitisha viwango wastani vya kuelewana.

Hali imeelezwa vizuri na Wolff(1964) ambaye anasema,

> "*Niwazi kuwa kama kuna mengi kuliko mfanano wa kiisimu yanayowezesha kuweko kwa mafanikio ya mawasiliano baina ya lahajaa mbili .(tafsiri ni yetu)*

Msomi huyu anaendelea kueleza kuwa mfanano wa kiisimu wa kifonemiki,kimofemiki na kileksika baina ya lahaja mbili sio hakikisho kuwa kuna mlingano wa kiisimu baina ya lahaja hizo.Vilevile kuweko kwa mawasiliano baina ya lahaja mbili sio hakikisho kuwa kuna mlingano wa kiisimu baina ya lahaja hizo.

Kwa upande mwingine ,tukizingatia lahaja za Kiisukha na Kilogooli ,tunapata kuwa wazungumuzaji wa lahaja hizi wanaishi ka karibu kijiografia .Kwa hivyo kuna maingliano mengi miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja hizi hasa katika mambo ya dini na biashara .Hii inatokana na wazo kuwa kwa vile Walogooli hawana mashamba makubwa na idadi yao ni wengi wao hujiusisha na biashara ndogondogo katika masoko yanayomilikiwa na Waisukha kama vile Khayega na Shinyalu.

Kutokana na mahusiano haya mema ,wazungumzaji wa lahaja hizi hujaribu kadri iwezekanavyo kuzungumza au kuelewa lahaja za wenzao ,yaani, Waisukha hujaribu kuelewa au kuzungumza Kilogooli na wakati huo Walogooli hujaribu kuzungumza na kuelewa kiisukha ili kurahizisha mawasiliano na kuendeleza uhusiano mwema uliopo baina yao .Kwa hivyo hakuna matatizo mengi ya kimawasiliano miongoni mwa wazungumzaji wa lahaja hizi katika kiwango hiki.

Licha ya kutokua na na shida nyingi ya kimawasiliano na Walogooli ,wazungumzaji wa Kiisukha hawachukuliwi vyema na wazungumzaji wa lahaja hizo zingine.Wengi wa wahojiwa wa lahaja za Kikisa na Kibukusu walidai kuwa Waisukha ni watu walio na kiburi ,wakali,wenye hasira kubwa ,wenye kupenda vita na waliozungumza kwa haraka haraka,mambo yaliyowafanya wazungumzaji wa lahaja hizi zingine kuwaogo**pa na** hata kukosa kuwaelewa kwa urahisi.Wazungumzaji wa Kibukusu na Kikisa walidai kuwa sifa za Waisukha kuwa wakali ,wenye hasira na wenye kupenda vita ,zimewafanya wao kuogopa kutangamana nao kwa njia mbalimbali kwa kuwa walikua na hofu ya kuumizwa na waisukha na kwa hivyo ,ni vigumu kwao kujifunza kuwasiliana kwa lahaja hiyo .Vilevile ,walidai kuwa ,kuzungumza kwa harakaharaka na kwa njia inayoonyesha ukali kumeifanya lahaja hiyo ya Kiisukha kuwa ngumu kuelewa na hata kuwasiliana nayo.

Tukigeukia lahaja ya Kikisa, tunapata kuwa wengi wa wazungumzaji wa lahaja hizo zingine waliohojiwa yaani,Waisukha,Walogooli na Wabukusu walionyesha kutokuwa na

shida na wazungumzaji wa lahaja ya Kikisa.Hata hivyo,Wabukusu wanawachukulia kuwa wao ni Wakakamega ambao ni tofauti na Wabukusu lakini licha ya hao Wabukusu waliawafaa kuliko Waisukha.

Wakati huohuo ,Wakisa wenyewe walijiona kama wazungumzaji wa lahaja wastani ya Kiluyia wakiwa pamoja na Wawanga na Wamarama,jambo ambao limezungumziwa na wasomi wengine kama vile Itebete(1974). Kwa ujumla ,wengi wa waliohojiwa walionyesha kuelewa lahaja ya Kikisa baada ya lahaja zao za kwanza kama inavyojitokeza katika jedwali ifuatayo:

Asilimia ya uelewaji wa lahaja(%)

| zungumzaji wa lahaja | kiisukha | kikisa | kibukusu | kilogooli |
|---|---|---|---|---|
| ıkha | | | | |
| va sana | 100 | 5 | _ | 5 |
| va kwa wastani | _ | 65 | _ | 50 |
| va kidogo | _ | 33 | 100 | 45 |
| sa | | | | |
| va sana | _ | 100 | _ | _ |
| va kwa wastani | 48 | _ | 5 | 40 |
| va kidogo | 52 | _ | 95 | 60 |
| ıkusu | | | | |
| va sani | 5 | _ | 100 | _ |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| a kwa wastini | 10 | 45 | _ | 5 |
| a kidogo | 85 | 55 | _ | 95 |
| <u>ıooli</u> | | | | |
| ıa sani | _ | _ | _ | 100 |
| ıa kwa wastani | 65 | 35 | _ | _ |
| ıa kidogo | 35 | 65 | 100 | _ |
| | | | | |

Licha ya tofauti hizi, wengi wa wazungumzaji wa lahaja hizi nne yaani Kiisukha ,Kikisa, Kibukusu na Kilogooli walieleza kuwa wao hujaribu kadri wawezavyo kuwasiliana katika lahaja zao mbalimbali za kiluyia wanapokutana na kutaka kuwa na mawasiliano ya kawaida .Vilevile ,hulazimika kuzitumia lahaja hizo wanapokuwa na wazungumzaji wengine wasio Waluyia na wangependa kuzungumzia jambo la kisiri ambalo wasingelipenda watu hao wengine wasilijue.

Kwa muhtasari hayo ndiyo baadhi ya maswala ya kiisimu jamii yaliyo jitokeza katika utafiti wetu uliozingatia lahaja hizi nne.

## HITIMISHO

Baada ya kuzichunguza lahaja hizi nne za kibaluyha yaani Kiisukha, Kilogooli, Kibukusu na Kikisa, tukiwa na nia ya kuonyesha .

Matatizo ya kuelewana kimaongezi yanayotokea wakati watu wanaozungumza lahaja hizi wanapowasiliana, tumeweza kufikia maamuzi yafuatayo.

Kwanza ni kuwa tumeweza kudhirisha ya kuwa ni kweli kwamba yapo matatizo mbalimbali yanayotokea wakati watu wa lahaja hizi wanapoasiliana kimaongezi .Baadhi ya matatizo haya ni kuwa katika kiwango cha kilekisa kitajwa kimoja chaweza kuwa na msamiati tofauti katika kila lahaja .Pia neno /msamiati unaotumiwa kuonyesha kitajwa kimoja katika lahaja moja unaweza kuwa na maana tofauti katika lahaja moja unaweza kuwa na maana tofauti katika lahaja nyingine .

Katika kiwango cha fonetiki, tumedhihirisha kuwa ukosefu wa baadhi ya sauti katika lahaja moja na kupatikana kwa sauti hiyohiyo katika lahaja nyingine ni jambo ambalo hutatiza mawasiliano miongoni mwa wazungumuzaji wa lahaja mbili tofauti na mara nyingi hulazimisha watu wa lahaja hizo tofauti kuzingatia muktadha ili kuweza kuelewa maana .

Tumezingatia pia kiwango cha mofolojia ambapo tumeona kuwa kuwepo kwa tofauti za viambishi awali katika aina mbalimbali ya maneno na hasa vitenzi kumesababisha

kutoelewana kwa wazungumzaji wa lahaja hizi nne yaani Kiisukha ,Kilogooli ,Kibukusu na Kikisa

Mwisho,tulizingatia swala la kisimu – jamii ambapo imejitokeza wazi kuwa misimamo \ taasubi mbalimbali inayoshikiliwa na wazungumzaji hawa huathiri mawasiliano.Imedhihirika wazi kuwa ukosefu wa kuelewana baina ya wazungumzaji wa lahaja mbili ambazo zina uhusiano au kukaribiana kiisimu ni ishara ya kuwepo kwa vipenge hasi (negative factors) vinavyozuia mawasiliano baina ya wazungumzaji wa lahaja hizo kama vile shutuma \ madai yanayoshikiliwa na wazungumzaji wa lahaja moja dhidi ya wenzao na yaliyodumu ingawaje hayana msingi madhubuti (stereotypes)

Hata hivyo, ni muhimu kutaja hapa kuwa matatizo haya yamejitokeza kuwa ya viwango tofauti. Kwa mfano tukizingatia tofauti za kileksika na zile za kiisimu jamii ambapo tilitumia takwimu kadha ili kukadiria tofauti zilizopo, imejitokeza wazi katika utafiti wetu kuwa , katika kiwango cha isimu jamii tofauti zilizopo ni kubwa kuliko zile za kileksia . Lakini ungependa kusisitiza kuwa tofauti hizi huenda zilitokea kwa sababu tulipozingatia swala la isimu jamii tulitumia idadi ya watu fulani kama sampuli yetu na kutegemea sana maoni yao kuhusu uwelewaji wao wa kila lahaja kinyume na utafiti wetu wa kileksika ambapo maneno yanayofikiriwa kuwa ya kimsingi yaliweza kufanyiwa utafiti mahususi wa kiisimu.

Kwa upande mwingine, hatukuweza kutumia takwimu kukadiria tofauti za kifonetiki na kimofolojia, lakini tumefanikiwa kuonyesha jinsi

Tofauti za sauti (ambazo tumeshughulikia sana katika sura ya pili) na tofauti za viambishi zimesababisha kuweko kwa matatizo ya kuwasiliana kimaongezi.

Kwa mujibu wa maelezo tuliyoyatoa hapa juu, ni bayana kwamba nadharia tete tulizokuwa nazo hapo awali, na ambazo zilikuwa kichocheo cha utafiti wetu zimedhibitishwa. Tumeonyeshwa katika tasnifu hii kwamba,

i)Tofauti za kileksika zimechangia katika kutatiza mawasiliano ya kimaongezi mwa wazungumzaji wa lahaja hizi za kiisukha, kikisa, kilogooli na kibukusu.

ii) Miundo tofauti ya kimofolojia na kifonetiki pia hutatiza mawasiliano miongoni wa wazungumzaji wa lahaja hizi za kibaluyia.

iii)Taasubi zinazoshikiliwa na watu wanaongea lahaja hizi za kibaluyia, zimechangia katika kurahisisha au kutatiza mawasiliano miongoni mwa wazungumuzaji wa lahaja hizi.

Ikiwa msomaji wa tasnifu hii atayaona haya yote, basi hatuna budi kuridhika kwamba ungo kuu la uchunguzi huu limetimizwa.

Mwisho kabisa, tungependa kusisitiza kuwa kazi hii ni kama kichocheo kwa wasomi wengine ili waweze kuzifanyia lahaja zingine za kibaluyia na lugha nyingine utafiti zaidi kwa kuzingatia vipenge mbalimbali katika lahaja hizo

## MAREJELEO


Abercrombie, D (1967): Elements of General Phonetics
Edinburgh. Edinburgh university press.

Angogo. R.K (1983): Unity in Diversity: A Linguistic of Western Kenya
Beitrage Zu Africanistic Band 20.

Brown G. (1972) : Phonological rules and Dialect variation:
A Study of the Phonology of Lumasaaba.
Cambridge . Cambridge University Press.

Byron. T (1977): Historical Linguistics, (Cambridge)
Cambridge University Press.

Cole, D.T (1967): Some Features of Ganda Linguistic Structure
Johannesburg Witwatersrand University Press.

Dalgish. G.M(1978): The morphonophonemics of Olutsotso: Issues and Implications
Tasnifu ya Phd, Chuo Kikuu cha illinoise.

Gichoni W. (1999): Sarufi fafanuzi ya Kiswahili
Nairobi Longhorn.

Gudschinsky,S: The ABC's of Lexicostatistics katika Hymes, D(ed)(1964):
Language in Culture and Society, News York.
Harper and Row publishers

Guthrie. M. (1967) The Classification of Bantu Languages,
London, Dawsonsa Pall Mall.

Hjelmslev (1970): Language an Introduction.
London. University of Winsconsin press.

Itebete P.A.N (1974):" Language Standardization in Western Kenya;
The Luhya Experiment" katika
Whiteley (ed) 1974:87-114

Johnson H (1919): A comperative Study of the Bantu and Semi- Bantu
Languages. Oxford. The Elanderon Press.

Kasaya, S.Z (1992): Logooli, Wanga and Lubukusu dialects of Luyha
A study of Major Phonological Process,
Tasnifu ya M.A Haijachapishwa. Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Ladefogled (1970): Language in Uganda. Nairobi. Oxford University Press.

Lambert, W.E et al (1968):A Study of the roles of attitude and motivation
In second language learning. Katika
Fishman, J.A ed (1968B).

Lambert, W.E (1963): Psychological approaches to the study of languages
Modern Language journal.

Laver J (1994): Principles of Phonetics,
Cambridge, Cambridge University Press.

Lehmann, P.W (1973):Historical Linguistics;An introduction
New York. Holt Rinehart and Winston.

Lidonde. A. (1976): A Generative Phonology of Lwitakho.
Tasnifu ya M.A Haijachapishwa Chou Kikuu Cha
Nairobi.

Makila, F.E (1978): An Outline History of the Babukusu of Western Kenya.
Nairobi. Kenya Literature Bureua.

Mbaabu, I (1992): Sarufi ya Kiswahili
Nairobi .Longhorn.

Mebo. P. (1989): The Lwisukha Noun Phase: A syntactic Analysis. Tasnifu ya M.A
Haijachapishwa. Chuo Kikuu Cha Nairobi

Mgullu R. (1999): Mtalaa wa Isimu ; Fonetiki, Fonologia na Mofolojia
Nairobi Longhorn.

Milroy, L (1980): language and Social Networks.
London. Basil Blackwell.

Mojola, A.O (1998): God Speaks in our own Languages.
Nairobi . Bible Society of Kenya.

O'connor. J.D.(1973):Phonetics. London Penguin Group.

Osogo J. (1966): A History of the Baluyha,
Nairobi. Oxford University Press.

Richards,J.et al (1985):Dictionary of Applied Linguistics.
Harlow .Longman

Roach, P. (1983): English Phonetics and Phonology.A practical course. New York Cambridge University Press.

Samarin , J.W(1976): Field Linguistics. A Guide to Linguistic Field Work New York. Holt Rinehart and Winston.

Seligman,C,et al (1973):The Effects of Speech Style and Other attributes on teachers attitude towards pupils in Language in Society pgs 131-142

Swadesh, M. (1955): Towards Greater Accuracy in Lexicostatistics Dating, New York. IJAL 21;121-137.

Troike M,S (1989): The Ehnography ofCommunication ; An introduction Oxford . Basil Blackwell.

Were. G.S (1967): A History of the Abaluyia of Western Kenya . Nairobi East Africa Publishing House.

Westerman,Dr and Ward. I(1970): Practical Phonetics for Students of African Languages, London Oxford University Press.

William (1973): " A Subgrouping of the Luhya group" A paper read at the 4th annual linguistics New York; SUNNY.

Wolff .H "Intelligibility and inter-ethnic attitude" katika Hymes, D. ed (1964) Language in Culture and Society. New York. Harper and Row Publishers.